
MID WEEK JACKPOT!
TZS. 508,027,160
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Afa** akidaiwa kujirusha toka kwenye ghorofa Stendi ya Magufuli

UKURASA 2




UKURASA 9

Nipashe
MWANGA WA JAMII
Jumapili Machi 12, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • No. 0581247
www.ippmedia.com
JUMAPILI
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Kufuru ya ulawiti

• **Kituo** cha Polisi charekodi matukio 20 ukatili dhidi ya watoto kila wiki... *Endelea Ukurasa 2*



Shughuli za wafanyabiashara zikiwa zimesimama kwenye mitaa mbalimbali ya eneo maarufu la biashara Afrika Mashariki la Kariakoo, Dar es Salaam baada ya kufunga biashara zao jana asubuhi ili kushiriki kongamano lililoandaliwa na Mkuu wa Mkoa huo, Amos Makala (hayupo pichani), kitendo kilichosababisha usumbufu kwa watu waliofika kupata mahitaji kutoka maeneo ya mbali. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

UKURASA WA 3

### ACT YAMULIKA JAMBO NYETI MCHAKATO WA KATIBA MPYA

MWENYEKITI wa Chama cha ACT Wazalendo, Juma Duni Haji amesema mchakato wa upatikanaji wa Katiba Mpya unapaswa kukamilika kabla ya kwa uchaguzi mkuu wa mwaka 2025, ili wananchi waongozwe na watu...

## Mbowe: Hakuna kuachiana majimbo

UKURASA 3

MIAKA MIWILI IKULU

## Samia awekeza jipya diplomasia inayotakasisha siasa nchini

UKURASA 4



Rais Samia Suluhu Hassan akimwapisha Dk. Wilson Mahera kuwa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Ikulu Chamwino, Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

MICHEZO SIMBA YAIRARUA MTIBWA UK. 24 MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA

# Afa akidaiwa kujirusha toka ghorofani Stendi ya Magufuli

**Na Christina Mwakangale**

MWANAMUME ambaye jina lake halijafahamika, amefariki dunia baada ya kudaiwa kujirusha kutoka ghorofa ya tatu kwenye jengo la Stendi Kuu ya Mabasi ya Magufuli iliyoko Mbezi Louis mkoani Dar es Salaam.

Tukio hilo lilitokea jana asubuhi na kusababisha taharuki kwa watumiaji wa kituo hicho ambacho husafirisha abiria wa ndani na nje ya nchi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, Kamishna Msaidizi wa Polisi Mtatiro Kitinkwi aliithibitishia Nipashe jana kutokea kwa tukio hilo ambalo alisema lilitokea majira ya saa mbili asubuhi kituoni huko.

"Ni kweli tukio limetokea majira ya saa 2:30 asubuhi kwenye Stendi ya Magufuli na mtu huyu ambaye ni mwanamume, hajatambulika kwa jina. Anakadiriwa kuwa na umri wa kati ya miaka 42 na 45.

"Amejirusha kutoka ghorofa ya tatu na kufikia kichwa. Mwili wake umehifadhiwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) Tawi la Mloganzila," alifafanua.

Kamanda Mtatiro alisema uchunguzi wa kifo hicho unaendelea ikiwa ni pamoja na kubaini jina lake.

Bingwa Mwandamizi wa Afya na Magonjwa ya Akili MNH na Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wataalamu wa Afya ya Akili Tanzania (MEHATA), Dk. Saidi Kuganda alisema sababu kuu ya matukio ya mtu kutenda hivyo huwa ni magonjwa ya akili na msongo wa mawazo.

# Wachimbaji dhahabu wafa

**Na Romana Mallya**

WACHIMBAJI wadogo wanane kati ya tisa wa dhahabu waliokuwa wanachimba madini hayo kwenye Kijiji cha Igando, Kata ya Magenge wilayani Geita, wamepoteza maisha baada ya shimo walilokuwa wanachimba kujaa maji ya mvua.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita, Safia Jongo amethibitisha kutokea kwa vifo hivyo vilivyotokea usiku wa kuamkia jana.

Alisema vifo hivyo vimetokana na mvua inayoendelea kunyesha mkoani humo.

Kamanda Safia alisema kuwa eneo hilo ni lenye leseni ya utafiti na wachimbaji wadogo wanapoona hivyo, walivamia na kuanza kuchimba bila kufuata utaratibu.

"Taarifa hii ya kuwapo wachimbaji hao tuliipata usiku wa kuamkia leo (jana) majira ya saa tisa, tulipopata taarifa tulifanya vikao na diwani wa Magenge, Wilaya ya Geita.

Kamanda alifafanua kuwa mmoja wao alitoka kutoa mchanga juu ndipo alipoona maji yanaingia shimoni na wakati anarudi ili kuokoa wenzake ilishindikana.

"Huyu ndiye aliyetoa taarifa kwa wachimbaji wenzake wadogo kuwapo kwa wenzake chini. Kwa kuwa waliingia pale kwa jinai, hawakutoa taarifa polisi, tukio la tangu saa tisa tumekuja kulipata saa 10 alfajiri ya leo (jana) ndipo juhudi za kuwaokoa zikaanza.

"Mpaka asubuhi leo (jana) walipatikana saba na jioni hii tumempata mmoja kwa ushirikiano na Kikosi cha Zimamoto Mkoa wa Geita, jumla waliofariki dunia ni wanane na mmoja aliyetoa taarifa amekimbia," alisema.

Kamanda huyo alisema kuwa wote waliofariki dunia ni kutoa Kijiji cha Iparamasa na umri wao ni kati ya miaka 25 na 53.



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye (kushoto), akijadiliana jambo na Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Minara Tanzania, Gordon Porter, baada ya kutembelea kampuni hiyo, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Waziri Nape, aliipongeza kwa uwekezaji kwenye teknolojia inayowezesha ufuatiliaji wa minara ya simu hapa nchini kwa njia ya mtandao. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kufuru ya ulawiti watoto

**Na Mary Geofrey**

MKUU wa Dawati la Jinsia Mkoa wa Kipolisi Ilala, Dk. Christina Onyango amesema wanapokea kesi zaidi ya 20 kila wiki za matukio ya ukatili wa kijinsia, nyingi zikiwa ni ulawiti na unajisi kwa watoto.

Dk. Christina ambaye pia ni Mratibu wa Kituo cha One Stop Center Amana, amebainisha kuwa kwa mwezi wanapokea takribani kesi 100 kituoni huko.

Aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam alipotoa elimu ya ukatili wa kijinsia kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Jamhuri iliyoandaliwa na Umoja wa Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA) kupitia Taasisi ya Sauti ya Matumaini (SAMAF) wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.

Akizungumza na wanafunzi hao zaidi ya 600, Dk. Christina aliwataka kujiamini na kuripoti vitendo hivyo mapema ili kudhibiti kukithiri kwa kufuru hiyo nchini.

"Changamoto kesi zinazokuja zinazohusisha masuala ya kifamilia huwa zinakwama njiani kwa sababu wanakwenda kuzimalizia nyumbani, jambo ambalo sio sahihi na ndio maana vitendo hivi vinaendelea kuwapo.

"Nitoe wito kwa jamii wasifumbie macho vitendo hivi, waviripoti na wasikubali kumalizana nyumbani kwani tutakaposhirikiana na wakafikishwa mahakamani itasaidia kuvipunguza," alisema.

Dk. Christina pia aliwaasa vijana hao kuacha kujihusisha na vitendo vya ngono katika umri mdogo kwa kuwa ni chanzo cha maradhi.

Vilevile, aliwaonya dhidi ya tabia za kutazama picha za ngono kupitia simu, kwenda mabanda ya TV, kujihusisha na michezo ya kubahatisha na kamari pamoja n tabia nyinginezo zinazowaingiza kwenye vishawishi vya kufanya ngono. "Jiepusheni na tamaa, ridhikeni na kile ambacho wazazi wanawapatia ili msije kujiingiza kwenye matendo mabaya ikiwamo ya kujiuza kwa sababu urithi wa kudumu na wenye faida ni elimu. "Na mnapofanyiwa ukatili usikimbilie nyumbani, wahi hospitalini au polisi. Hii itatusaidia kupata ushahidi wa awali pamoja na dawa za kuzuia maambukizi au mimba," alisisitiza Dk. Christina. Mtendaji Mkuu wa umoja huo, Penina Malundo alisema lengo la kufikia wanafunzi hao ni kutoa elimu ya kujitambua na kuwaepusha na vishawishi rika ambavyo vitasababisha kukatisha ndoto zao.

"Leo tumekusanyika hapa kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani kwa kutoa elimu ya masuala mbalimbali ikiwamo ukatili wa kijinsia na hedhi salama kwa wanafunzi," alisema.

Alifafanua kuwa vitendo vya ukatili wa kijinsia vimekuwa tishio kubwa nchini na kufifisha ndoto za vijana wengi, hususani wanaokuwa shuleni na kuwafanya wakatishe masomo yao.

"Wengi wao wanakatisha masomo kutokana na aibu wanayopata baada ya kufanyiwa vitendo hivyo, wengine kupata majeraha mbalimbali ya kimwili na kifikra ambayo wanaona hawana nafasi tena ya kurudi shuleni.

"Sasa ni wakati wa jamii kusimamia pamoja kuhakikisha tunazidi kupaza sauti zetu hadi vitendo hivi kutokomezwa kabisa," alisema Penina.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Jamhuri, Boniphace Mwalengo aliwashukuru waandishi wa habari hao na Jeshi la Polisi kwa kutoa elimu hiyo itakayosaidia kuleta mabadiliko kwa wanafunzi hao.

Mmoja wa wanafunzi hao, Athumani Ngoda alisema: "Vitu vingi nilikuwa sivifahamu kama namna gani ninaweza kusema kama kuna ndugu anataka kunibaka au kunilawiti na je, niende wapi? Ninashukuru kupitia elimu hii tuliyopewa nimevielewa na nitavifanyia kazi".


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......19/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: RAMADHANI ABDALLAH WA MJI MKUU**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA: ANUNI RAMADHANI CHASAMBO**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 13 Mwezi 03 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehem anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

**Imetolewa leo tarehe 09 mwezi 03 mwaka 2022**

HAKIMU

**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**ELIZABETH CONSTANTINO MAKOMBE** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **SANLG** yenye usajili namba: **MC383 AKV, CHASSIS NAMBA: LBRSPKB56E9000477 na ENGINE NAMBA:14925407.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/92239/2023**

**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**MIRAJI JUMA BARUTI** anatangaa kupotea kwa kadi ya pikipiki ana ya **BAJAJ BOXER** yenye usajili namba: **MC602 BXZ, CHASSIS NAMBA: MD2B15BY3JWL87884 na ENGINE NAMBA: JVZWJL18157.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA : **ARU/ARU/RB/92399/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......32/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: EVA DAVID KAMWELA WA TUNGI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA: WILFRED MEKA MASAWE**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 17 Mwezi 03 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehem anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

**Imetolewa leo tarehe 09 mwezi 03 mwaka 2022**

HAKIMU

**IN THE DISTRICT DELEGATE OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE & ADMINISTRATION CAUSE NO.7 OF 2023**
**In the matter of the estate of the late**
**FATUMA MIRAJI MSUYA**
**And**
**In the matter of an application for letters of administration by YUDA DONASIANI TARIMO.**

**GENERAL CITATION**
**(Made under Rule 75 of Probate Rules, (Cap 352 R.E.2002)**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above- named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above- named Petitioners.

Objections to the grant should be filed on or before the **13 Day of 3, 2023**

**Dated at Dodoma this 2 day of 3, 2023**

RESIDENT MAGISTRATE

## HABARI KITAIFA




Ofisa Utumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mkoa wa Kinondoni, Mwanahamisi Ibrahim (wa tatu kulia), akikabidhi zawadi mbalimbali kwa Msimamizi wa Huduma za Wagonjwa wa ndani wa Hospitali ya CCBRT, Rehema Mahimbo, wakiadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Mbowe: Hakuna tena kuachiana majimbo

**Na Romana Mallya**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe amesema wanataka kurejesha heshima ya chama chao kwenye mikoa mitano ya Ukanda wa Pwani, ambayo kwa kipindi kirefu ilikuwa kama ngome ya Chama cha Wananchi (CUF).

Amesema huko nyuma waliamini katika kuunganisha vyama lakini adhma hiyo mara nyingi imekutana na misukosuko kwa sababu mbele ya safari baadhi ya wenzao wamekuwa wanakengeuka.

Akizungumza jana mkoani Dar es Salaam baada ya chama hicho kupokea wanachama wapya, Mbowe alisema wamejipanga kuingia kwa miguu yote miwili kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Tanga, Lindi na Mtwara.

Alisema kuwa kwa miaka mingi safari ya kukijenga CHADEMA ilianzia alikokuita Bara, wakiamini zaidi katika ushirika.

"Tuliona Ukanda wa Pwani umeshikwa zaidi na wenzetu wa CUF, tukaamini katika kushirikiana na kuuacha ukanda huo kama ulivyokuwa.

"Tuliamini sana katika kuunganisha vyama na CHADEMA kwenye Katiba yetu kuna ukurasa unazungumza, CHADEMA ni chama ambacho kitajitahidi kuunganisha vyama.

"Adhma yetu hii mara nyingi imekutana na misukosuko kwa sababu wenzetu mbele ya safari hukengeuka, hatimaye CHADEMA tumesema wajibu wetu tutaufanya si kwa kuunganisha vyama, tutaufanya kwa kuunganisha wanachama au wananchi wenyewe," alifafanua.

Mbowe alisema kuwa badala ya kuunganisha vyama ambavyo havina dhamira moja, wameona kwa hilo wanapoteza muda kwa kuwa wananchi wanahitaji chama imara, chama mbadala na umoja.

Alisema watazunguka kila kijiji, kata, kitongoji, mtaa kwa kugonga kila nyumba ili kukiandaa chama kwa ajili ya ushindi mkubwa mwaka 2025.

Kuhusu wanachama wapya, Mbowe aliwataka viongozi ndani ya CHADEMA wawapokee na kusisitiza kwamba yeyote atakayewazuia kwa sababu ya kuhofia nafasi yake itaondoka, 'ataondoka kweli'.

"Hawa ni Watanzania wenzetu, wapewe jukwaa wafanye siasa, Dar es Salaam ina kata 102, ina majimbo 10 ya uchaguzi, ina mikoa mitano ya kichama, ina mitaa 566, ninyi mtaingia kwenye Operesheni ya Kanda ya Pwani.

"Tunawahitaji, tutawatumia na ninyi mtakitumia chama kufanya kazi ya wananchi. Mageuzi makubwa ya kila chama cha siasa duniani huanzia makao makuu ya jiji kubwa.

"Kwa kushirikiana nanyi, tunataka tuibadilishe Dar es Salaam kabisa! Tulifanikiwa kwa kiwango kikubwa mwaka 2015, tukapata wabunge, mameya, naibu meya na madiwani, mwaka 2020 walichakachua, hapo katikati mwendazake akafanya yake yakaenda hivyo," alisema.

Mbowe alidai kuwa kwa muda mrefu, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kiliamua kuanzisha vyama vingi ili kuwatenga.

"Wakoloni walisema 'ukitaka kutawala taifa, watenge uwatawale'. Tukajitenga makundi madogomadogo, kundi moja linaitwa CUF, kundi lingine linaitwa CHADEMA, lingine NCCR, TLP, vyama 20 vya kazi gani?

"Vyama vingine vimeundwa kwa kuegeshwa ili vilete mpasuko katika vyama vya upinzani, tunaona viongozi wetu wanakwenda vizuri, wanafika mahali wanakengeuka.

"Wanabadilisha msimamo bila kuwaambia wanachama, vyama vyao vinaingia katika migogoro, CHADEMA tutaendelea kusimama imara wakati wote, mliokuja, njooni tujenge siasa safi, siasa ya haki," alisisitiza.

Aliwaahidi kwamba watapata fursa kama mwanachama mwingine yeyote ndani ya CHADEMA anavyopata.

"Ninyi ni wanachama kama alivyokuwa Mbowe, mna haki kama aliyokuwa nayo Mbowe. Hata mkitaka kugombea Mwenyekiti Taifa, karibuni, haina shida.

"Hakuna atakayebaguliwa kwa dini au imani yake, uwe na dini au usiwe na dini, hiki chama kipo Tanzania nzima, kinaunganisha makabila ya mikoa yote," alisema.

Kiongozi huyo pia alisema waliopo ndani ya chama na walioingia, wote wana haki CHADEMA.

Alisema wamekijenga kwa gharama kubwa na wapo waliopoteza maisha, kupoteza viungo, kufungwa na wengine kupotea.

"Tumepata madhila ya kila aina lakini tulikataa kutolewa kwenye mstari, dhamira yetu ni kuijenga Tanzania moja yenye kuangalia ustawi wa kila mmoja wetu, haijawahi kubadilika," alisisitiza.

Mbowe alisema amefarijika kuona waliojiunga na chama hicho jana, wanatoka kwenye ukanda wa mwambao wa Bahari ya Hindi.

Wanasiasa 384 waliojiunga na CHADEMA jana wakitokea CUF ni pamoja na aliyekuwa Mkurugenzi wa Habari na Uenezi wa chama hicho, Abdul Kambaya.

Wengine ni pamoja na Saad Issa aliyekuwa Ofisa Makao Makuu CUF, Salma Majere, aliyekuwa Ofisa Mambo ya Nje wa CUF, pia aliwahi kuwania ubunge wa Kinondoni na viongozi wa kata za Tandale, Makumbusho, Ndugumbi, Magomeni, Mwananyamala na Temeke.

# ACT yamulika jambo nyeti mchakato wa Katiba Mpya

**Na Julieth Mkireri,**
TANDAHIMBA

MWENYEKITI wa Chama cha ACT Wazalendo, Juma Duni Haji amesema mchakato wa upatikanaji wa Katiba Mpya unapaswa kukamilika kabla ya kwa uchaguzi mkuu wa mwaka 2025, ili wananchi waongozwe na watu waliowachagua kwa ridhaa yao.

Amesema mpaka sasa serikali haijaweka hadharani kauli ya lini mchakato wa sheria ya mabadiliko ya katiba utawasilishwa bungeni kwa ajili ya kutoa fursa ya sheria hizo kutumika katika upatikanaji wa Katiba Mpya.

Duni alitoa kauli hiyo jana akiwa Tandahimba mkoani Mtwara wakati wa ziara ya kutambulisha ahadi za chama chama chao kwa wananchi.

Alisema hawawezi kwenda kwenye kura ya maoni kubadilisha Katiba Mpya wakati hadi sasa mfumo uliopo ni wa amri na uamuzi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Baada ya Rais kujibu hoja za wapinzani kuhusiana na mabadiliko ya siasa za kidemokrasia, hoja kuu iliyojitokeza ni mabadiliko ya katiba na vyama vya upinzani walielezea hili kwa kutaka sheria ya uchaguzi, sheria ya vyama vya siasa, sheria ya polisi iliyokuwa inatusumbua sana wakati wa mikutano na sheria ya kura za maoni.

"Ili madai ya kutaka Katiba Mpya yaje kufanyika, ni lazima sheria hizi zote zibadilishwe kwenye Bunge na hili linatakiwa kufanyika kabla ya Bunge la Katiba," alisema Duni.

Aliongeza kuwa ACT Wazalendo wanataka sheria hizo zibadilishwe ili wapatikane wajumbe huru ya Tume ya Uchaguzi watakaokuwa na uadilifu na ambao wamechaguliwa kwa mifumo rasmi.

Alisema kuwa katika maoni ya chama hicho yaliyopelekwa kwa kikosi kazi cha Rais, wameelezea njia na hatua nzuri ya kufikia mabadiliko hayo na serikali inatakiwa kutumia mawazo hayo kwa ajili ya kuipata Tanzania iliyo bora.

"Tunataka utaratibu wa namna ya sheria hizo zitakavyobadilika ili ziwahi na kutumika katika uchaguzi wa serikali za mitaa 2024 na Uchaguzi Mkuu 2025, tunataka kuona sheria hizi zinaabadilishwa kwa kuanzia kupata baraka zake katika Baraza la Mawaziri.

"Sisi tumesema kule Zanzibar, Dar es Salaam, Tanga na hapa tunataka muda rasmi wa kufikia mabadiliko hayo," alisema Duni.

Waziri Kivuli wa Nishati wa chama hicho, Ishaka Mchinjita aliitaka serikali ipitie upya mfumo wa uagizaji wa pembejeo na namna ya kumfikia mkulima ili wakulima wanufaike na kilimo cha korosho.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
12.03.2023

## TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Alhamisi tarehe 16-03-2023 kampuni ya Mainline Carriers Ltd itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka Dar-Es-Salaam Port kuelekea JNHPP SITE, gari hiyo ina namba ya usajili:

**T 454 DYG / T 877 EAU**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 19.3 Upana - mita 6.90 Kimo - mita 4.60**

3. Njia itakayotumika: **BANDARI YA DAR ES SALAAM** hadi **JNHPP SITE** kupitia **KILWA ROAD, KIBITI, MLOKA.**

Gari itasafiri muda wa usiku (Kuanzia saa 06:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri) Kutoka Dar es Salaam Port mpaka Bungu.

Kutoka Bungu kwenda JNHPP Site gari itasafiri muda wa mchana ( kuanzia 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

MIAKA MIWILI YA RAIS SAMIA

# Awekeza jipya kwa staili diplomasia inayotakasisha siasa nchini, kimataifa

**Na Peter Orwa**

SASA ni miaka tisa imepita wakati kama huu, Samia Suluhu Hassan akachaguliwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge la Katiba nchini. Wengi hawakumfahamu kwa kina hata wajihi wake, zaidi ya hali ya kawaida.

Alikuwa na miaka 14 kwenye ulingo wa siasa na hasa ngazi ya juu, lakini sifa moja kuu amependa kwa kasi, akibeba sifa ya umahiri wa utendaji kiofisi.

Kadri alivyotumika kwenye Bunge la Katiba akiwa chini ya Mwenyekiti Samwel Sitta, akawa anatumika kwa staili ya hulka yake ya upole, mwenye maneno kidogo na matendo zaidi, wengi wakaanza kuvutiwa naye.

Akiwa meza kuu ya kuratibu mambo, akiwa na sura zingine ambazo hazikuwa maarufu sana kisiasa, akiwamo aliye sasa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, kuna jambo la kipekee linaonekana.

Walikuwa marafiki kikazi 'mkubwa na mdogo' katika meza, lakini kuna cha kuvutia kila mmoja anatumia muda mwingi akifanya kazi na masihara na waliotoka kambi ya upinzani, akiwamo marehemu Mzee James Mapalala, mwasisi wa chama CUF.

Baadaye, wastani wa mwaka mmoja na nusu wakati chama tawala CCM kinampitisha Dk. John Magufuli kuwa mgombea urais, akatangazwa Mgombea Mwenza wake ni Samia. Jamii ikazidi kufunguka macho ya ziada juu yake.

Ummy naye akaonekana kijana wake mchapakazi katika safu Baraza la Mawaziri, kwa wizara nyeti; Afya, pia TAMISEMI, aking'ara kwa uchangamfu wake uleule na 'ushapu' kazini.

Wote wakaingia kwenye kampeni kitaifa iliyojibu na ushindi wa mgombea wa chama tawala, Samia akichukua nafasi ya Makamu wa Rais.

Hiyo ikachukua wastani mwaka mmoja na robo, hadi kuliposhuhudiwa kifo cha mkuu huyo wa nchi awamu ya tano na mara moja, Dk. Samia akakabidhiwa nchi, kwa mujibu wa maelekezo ya Katiba kitaifa.

Kimsingi, Dk. Samia alianza kuonekana rasmi kwenye siasa mwaka 2000, alipoteuliwa Mbunge wa Viti Maalum, kukiendana na kiti cha Waziri wa Utalii na Biashara, katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Akachaguliwa tena Mbunge wa Viti Maalum, sambamba na kuwa Waziri wa Kazi, Jinsia na Watoto, hadi mwaka 2010 alipogombea ubunge Jimbo la Makunduchi, Unguja na alikoshinda uchaguzi.

Hapo ndipo akasikika mama huyo ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Muungano na Mazingira) na ilipotimu mwaka 2014, akachaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum la Katiba.




Siku Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alipohudhuria mkutano wa wanawake wa CHADEMA, Machi 8 mwaka huu. **PICHA: MAKTABA**

### KITI CHA URAIS

Akiangaliwa kwa kina hatua zake tangu Makamu wa Rais hadi sasa, ikiambatana na historia yake tangu Bunge la Katiba, Dk. Samia ni muumini wa maridhiano na urafiki kisiasa, hadi penye diplomasia ya uchumi.

Hata ikirejewa mkasa na kipindi Mbunge Tundu Lissu, kupigwa risasi na wanaodhaniwa walidhamiria kumuua, muda mfupi baada ya tukio, Dk. Samia akiwa Makamu wa Rais mkutanoni jijini Nairobi, Kenya, akafika hadi hospitalini kujumlia hali mgonjwa huyo. Hilo Lissu daima halifichi limemtia faraja sana.

Hapo ana nyongeza alipohojiwa na wanahabari, akienda mbali kwamba anampa hadhi ya dada yake, kwani kuna wakati Lissu akiwa waziri kivuli bungeni, dhidi ya Waziri Samia, walishirikiana kutaniana, huku akimpa heshima kubwa.

### MAISHA YA URAIS

Baada ya kukabidhiwa urais wa nchi, Rais Dk. Samia anashuhudiwa anaendesha harakati endelevu za namna mbili; kiuchumi na kisiasa, kwa staili ya kufungua milango yote ya ustawi anakodhani kumezibika.

Kisiasa akaanza na ahadi za kupatana na kukuza undugu kisiasa, akinyunyiza dawa stahiki kwenye kidonda, katiba mpya, ambayo nayo inaahidiwa si muda mrefu matendo yanaingia jikoni, kukidhi matakwa.

Mjadala ukiwa umenoga na kuwekwa msukumo wa uhuru wa mijumuiko ya kisiasa, 'kufumba na kufumbua' Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, aliyekuwa gerezani akituhumiwa jinai, akaachiwa na mara moja wakakutana kwa faragha kujadili hatima ya siasa ya nchi.

Ni mjadala uliopiga hatua, Rais Dk, Samia kukutana na viongozi wa vyama, simulizi iliyopiga hatua kufutwa mashitaka ya jinai yaliyokuwa yanamkabili Mbowe na baada ya siku moja, akamkaribisha kuteta naye katika mazungumzo ya muafaka na hatima ya siasa nchini.

Baadaye akiwa katika ziara ya mikakati ya kiuchumi, jijini Brussels, Uingereza, akakutana tena na mwanasiasa Tundu Lissu, Makamu wa Mbowe aliyekuwa uhamishoni nchini humo.

Lissu aliyeomba kukutana na Rais wake, baadaye akatoa taarifa 'mazungumzo yalikuwa mazuri', akisifu mchakato nchini kurejeshwa rasmi uhuru wa kujumuika kisiasa.

Ni aina ya hadithi zilizoambatana na Lissu kupatiwa maslahi yake anayodai akiwa mbunge. Simulizi kama hizo, zikasikika tena ndani ya wiki moja iliyopita kutoka vyanzo vya CHADEMA, chama hicho sasa kitalipwa ruzuku zake zote, sasa wastani wa shilingi bilioni tatu.

Mwaka huu ulipoanza, kukashuhudiwa Lissu aliyelalamika sana awali kadhulumiwa maslahi yake bungeni, pia hana uhakika wake nyumbani, leo anakiri vyote vimenyooshwa, katika zama za miaka miwili ya uongozi wa Awamu ya Sita.

### MAGEUZI

'Hayawi hayawi, yamekuwa!" Mwishoni mwa Januari iliyopita, ndipo akashuhudiwa Lissu anatua Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, Dar es Salaam, alikopokewa kwa shangwe na vigelegele, akisindikizwa na umati ulioambatana na wana - usalama, polisi hadi kwenye viwanja vya mkutano wilayani Temeke.

Hata hivyo, kutoishi kwake nchini kwa miaka mitano, mwaka 2020, Lissu alirejea na kugombea nafasi ya urais ambao hakushinda, kisha akaondoka mara moja kurejea Ubelgiji.

Ni mambo baadaye yaliyoambatana na kufutwa kesi za jinai dhidi yake, kama kilichotokea kwa Mbowe, vivyo ikisadikika na kisha kuthibitishwa kwa wengine wa kisiasa.

Ukapita muda mfupi, zikasika habari na hata kuthibitishwa na mhusika kwa tangazo lake, kuwa anarejea nchini mwezi huu, aliyewahi mbunge machachari jimbo la Arusha Mjini,Godbless Lema, hata baadaye 'akafunguka' kumshukuru moja kwa moja Rais Dk. Samia.

Akiwa amechelewa kwa siku kadhaa, Lema akatimiza ahadi yake kutua nchini Uwanja wa Ndege wa Kilimajaro (KIA) mwezi hu, akitokea nchini Canada alikokuwa uhamishoni.

Kama staili ilivyo kwa Lissu, akatikisa mjini na wapambe wengi wakiwamo maswahiba wa bodaboda na hadi sasa yuko ziarani mikutanoni, kama alivyofanya ndugu yake kisiasa, Lissu.

Mapokezi ya Lema yameweka rekodi, akiyaendeleza kwenye mikutano mingine ya hadhara. Iko wazi sasa Rais Dk. Samia, amebeba sifa kutoka kwa wanasiasa wa upinzani 'mama hana noma' naye akimwita huku Rais mikutanoni anamwita kwa jina 'mwanangu Lema'

Lililo kubwa hivi karibuni hata kuishangaza dunia, ni pale Dk. Samia akawa mgeni rasmi katika kikao cha Baraza la Wanawake Chadema (BAWACHA), pia wakiadhimisha siku ya kinamama kimataifa, ambako zilitolewa salamu za pande zote, kukiwapo kukaribisha ujumbe wa vyama vingine, ikiwamo CCM.

Ni kikao cha ufunguzi kilichotia fora, kila hatua kinamama hao 'kuwehuka' na ugeni wa Rais Dk Samia, wakati wa hotuba zote, yake akidokeza kadhaa ya siasa kujibu hoja, lakini kikubwa akawaambia ni shughuli ya mama, hivyo siasa waisubiri siku yake.

Hata katika neno lake awali, Mwenyekiti Mbowe, mara kadhaa akikiri uungwana wake wa kisiasa.

Dk. Samia, hakuwaacha hivihivi na kilio chao akiwadokeza kwa staili 'mboga' ya katiba mpya 'mchele sasa unachambuliwa'; suala liko njiani. Ni mvuto wa kisiasa uliowajumuisha wazito wa wana - CCM kikaoni na CHADEMA kirafiki.

Ni sura, matendo, hata kauli zinazofanana na kilichotamkwa kwenye kikao cha maridhiano kwa vyama vya siasa vyote nchini, Januari 3 mwaka huu.

Daima akasisitiza uhuru wa kuendesha siasa za ustaarabu, zimeanza kushuhudiwa, huku walioanza kampeni wanasifu usalama wanaopewa. Ni ishara njema, siasa kitaifa inazidi kutakata katika staili yake, kuelekea kilele zama za miaka miwili ya utawala wa Rais Dk. Samia.

# Wanafunzi 2,000 kunufaika vifaa vya kiteknolojia

**Na Frank Monyo**

ZAIDI ya wanafunzi 2,000 kutoka shule tano wilayani Korogwe wanatarajiwa kunufaika na msaada wa vifaa vya kiteknolojia na mawasiliano kutoka Taasisi ya Vodacom Tanzania Foundation.

Vifaa hivyo ni pamoja na kompyuta na tabiti zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 89. Msaada huo ni sehemu ya mradi wa taasisi hiyo wa kuziunganisha Shule wa African Child Project (ACP) kwa kushirikiana na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) unaolenga kuzifikia shule 300 nchini.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo, Mkuu wa Wilaya ya Korogwe, Jokate Mwegelo aliishukuru Vodacom Tanzania Foundation na washikirika wake, akisema msaada huo ni muhimu kwa kuwa utasaidia kubadili mfumo wa utoaji wa huduma wa elimu wilayani humo.

"Ninazipongeza jitihada hizi ambazo zitabadili mbinu za ufundishaji na namna wanafunzi wanavyojipatia nyenzo za kujisomea.

"Siku si chache tutaachana na mfumo wa utegemezi wa walimu na wanafunzi kutegemea vitabu kufundishia na kujifunza.

"Ujio wa mtandao wa intaneti na mifumo ya Vodacom kama vile E-Fahamu, walimu hawana haja ya kuwafundisha kila kitu wanafunzi bali kuwaongoza vile inavyopaswa.

"Kwa mwenendo huu, tunaamini Tanzania itakuwa miongoni mwa nchi zitakazotoa wanafunzi wabunifu wenye fikra pana. Tukiwa na wanafunzi wa aina hii, tutaweza kushindanishwa popote pale," alisema.

Alizitaja shule ambazo zimenufaika na msaada huo kuwa ni pamoja na Joel Bendera ambayo ilipokea kompyuta nane huku Mashewa, Ngombezi, Old Korogwe na Kwamndolwa zikipokea kompyuta sita kila moja pamoja runinga, tabiti na mashine ya kuchapishia.

Aliongeza kuwa shule zote zilizopokea msaada huo zitapokea mafunzo kuhusu namna ya kutumia mfumo wa kujifunzia wa e-Fahamu.

"Ninaomba tuwapongeze Vodacom Tanzania kwa ubunifu wao kwenye huduma za kidigitali katika sekta tofauti kama vile elimu, afya, fedha, kilimo na benki.

"Ni huduma ambazo zinagusa nyanja zote za maisha yetu. Ni fahari kwa serikali kuwa na mshirika kama ninyi ambaye huduma na bidhaa zake zinalenga kutatua changamoto zinazoikabili jamii.

"Nimefahamishwa kuwa programu ya m-mama tayari inapatikana mkoani Tanga ambapo inasaidia kuzuia vifo vitokanavyo na uzazi," alisema

Kaimu Mkurugenzi wa Uhusiano na Mawasiliano wa Vodacom Tanzania Foundation, Annette Kanora alianisha malengo ya mradi wa uunganishwaji wa shule huku akiipongeza serikali na washirika wake kwa kuunga mkono usambazaji wake nchini kote.

"Tumepokea ushirikiano wa kutosha na wa thamani kutoka serikalini na washirika. Kama kampuni, ajenda yetu ni kuwa kampuni inayoongoza katika dunia ya sasa ya kidigitali huku tukibadili Maisha kupitia teknolojia.

"Msaada huu ni uthibitisho wa jitihada hizo ambapo tunalenga kutoa maudhui kupitia jukwaa la mfumo wa e-Fahamu la Vodacom, kueneza vifaa vya Teknolojia ya Mawasiliano na Habari (TEHAMA) na kuziunganisha shule na mtandao wa intaneti nchini kote.

"Tunaamini hii haitachochea ueneaji wa huduma za kiditali, pia na ufanisi wa wanafunzi ambapo watakuwa na uwezo wa kuzifikia nyenzo nyingi za kujifunzia zaidi.

"Ninawaasa wanufaika wote wa mradi huu kuvitumia vifaa hivi tunavyowapatia leo (jana) ili kuboresha ufanisi kwenye shughuli zenu kwa manufaa mapana ya taifa letu," alisema Annette

Akitoa salamu kwa niaba ya shule zingine, Mkuu wa Shule ya Sekondari Joel Bendera, Mwalimu Msemwa aliwataka walimu wenzake kuhakikisha vifaa walivyokabidhiwa vinatumika kama inavyopaswa, pia kuvitunza ili kuwanufaisha wanafunzi na walimu kwa muda mrefu.

"Ningependa kutoa changamoto kwa wanufaika wote wa mradi huu kuanza safari ya mabadiliko ya kuachana na mbinu za ufundishaji na kujifunzia tunazozitumia sasa na kuhamia kwenye mfumo wa kidigitali.

"Tukiwa na ongezeko la idadi ya upatikanaji wa mtandao wa intaneti na umiliki wa simujanja, hakuna sababu ya kuendelea kutumia mifumo ya kizamani.

"Pia, tuvitumie na kuvitunza vifaa hivi ili kuwahamasisha wadau wengine kujitokeza zaidi. Kwa kuongezea, tuanze kujumuisha vifaa vya kiteknolojia na uunganishaji wa mtandao wa intaneti katika bajeti za mwaka za shule zetu ili kuendana na kasi hii," alisema Msemwa.

Programu ya e-Fahamu ilianzishwa na Vodacom Foundation mnamo mwaka 2017 kwa lengo la kuwasaidia walimu na wanafunzi kupata vitabu vya ziada na kiada kwa shule za msingi na sekondari ambayo inafuata mitaala ya kutoka maktaba ya Taasisi ya Elimu Tanzania na masomo ya kimataifa bure kwa njia ya mtandao.

Lengo la tovuti hiyo ni kuunga mkono juhudi za serikali za kutoa elimu bila malipo kwa shule za msingi na sekondari nchini.




Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Mhandisi Amani Mafuru akizungumza jijini humo juzi, baada ya kukabidhiwa msaada wa madawati 30 kutoka kwa Benki ya DCB, kwa ajili ya Shule ya Msingi Kifuru, ikiwa ni sehemu ya kampeni inayoendelea ya benki hiyo ya kusaidia elimu iitwayo 'Elimu Mpango Mzima na Mama Samia'. Wa pili kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa DCB, Isidori Msaki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadau nchi 30 kukutana Dar kujadili gesi asilia

**Na Romana Mallya**

WADAU wa gesi asilia kutoka nchi 30 duniani wanatarajia kukutana jijini Dar es Salaam kujadili na kutoa ushuhuda namna nchi zao zilivyochochea matumizi ya nishati safi ili kuleta chachu ya matumizi kwa Watanzania.

Mkurugenzi wa LPG Expo, Catherine Ho aliyasema hayo juzi mkoani Dar es Salaam alipozungumzia maonyesho ya gesi asilia ya kupikia yajulikanayo kama 'The East Africa LPG Expo - Tanzania 2023' yanayotarajiwa kufanyika kwa siku mbili kuanzia Jumatano ijayo.

Maonyesho hayo ambayo yatafanyika jijini Dar es Salaam, yameandaliwa na LPG Expo kwa ushirikiano wa Chama cha Wadau wa Gesi ya Kupikia Majumbani (LPG).

"Litakuwa ni moja ya matukio makubwa kikanda, litachochea mjadala wa nishati safi na kukuza matumizi ya gesi katika matumizi mbalimbali kwa maendeleo endelevu," Ho alisema.

Alibainisha kuwa LPG Expo imekuwa ikiandaa na kusimamia maonyesho na makongamano yanayohusiana na LPG kimataifa na imekuwa zaidi katika Afrika Magharibi na Asia na sasa inapenya ukanda wa Afrika Mashariki.

"Lengo ni kuunganisha sekta ya ndani ya LPG na wadau mbalimbali wa kimataifa wa LPG kutoka duniani kote ili kuwa na mazungumzo na mijadala ambayo pengine inaweza kuwa vigumu kuwa nayo.

"Tunaleta wataalamu wa kimataifa ili kutoa utaalamu na kushiriki utafiti ili kusaidia taifa mwenyeji kutambua changamoto zinazofanana na masuluhisho na mikakati inayowezekana ya kuendeleza sekta hii," alisema.

Aliongeza kuwa juhudi mbalimbali zilizofanywa miaka ya hivi karibuni zimewezesha kuwapo kwa ongezeko la matumizi ya LPG na kuifanya Tanzania kuwa kwenye nafasi nzuri ya kukaribisha maonyesho mfululizo yanayohusiana na hilo.

"Tunaamini huu ni wakati mwafaka kwa LPG Expo kuja kusaidia wawekezaji kuifahamu Tanzania kupata maarifa kuhusu soko hili linalostawi na kusaidia kuwa kiungo muhimu katika mnyororo wa kimataifa wa usambazaji wa LPG," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Chama cha Wadau wa Gesi ya Kupikia Majumbani, Amos Jackson alisema Waziri wa Nishati, January Makamba anatarajiwa kuyafungua maonyesho hayo.

Pia alisema kutakuwa na semina ambazo washiriki watajadili uzoefu wa matumizi ya gesi duniani kwa lengo la kuchochea utumiaji wa gesi asilia na watu kuachana na nishati chafu.

"Manufaa yake ni pamoja na Watanzania kusikia ushuhuda kutoka nchi mbalimbali duniani namna zilivyotoka kwenye matumizi ya nishati chafu ili nao waachane na matumizi ya nishati zisizo safi kama kuni na mkaa," alisema.


Jackson alisema washiriki hao pia watapata fursa ya kutangaza biashara zinazohusiana na vifaa na bidhaa ya gesi ya majumbani.

"Hii ni fursa nzuri kwa wafanyabiashara wote wanauhusika kwenye mnyoyoro mzima wa gesi ya kupikia majumbani kuweza kujifunza mambo mbalimbali yanayohusiana na bidhaa hizi," alisema.

Alibainisha mkutano huo unafanyika ukiwa ni mwendelezo wa jitihada za serikali baada ya ule uliofanyika mwaka jana ulioandaliwa na Wizara ya Nishati kwa lengo la kujadili kuhusu matumizi nishati safi, ukihudhuriwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema katika maonyesho hayo pia kutakuwa na uzinduzi wa Chama cha Wafanyabiashara wa Gesi ambacho kinalenga kuunga mkono jitihada za serikali za kukuza biashara ya gesi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII




# Tuchukue hatua kuukabili mmomonyoko maadili nchini

**RIPOTI** za vyombo vya habari nchini zina ishara zote za kuwapo shida kimaadili inayosababisha wingi wa matukio ya ukatili wa jinsia na mauaji ya watu.

Ukatili kijinsia unatajwa kushamiri kutokana na utandawazi, kwamba vijana wetu wanaona na kusikia mambo mengi yanayoendelea duniani, yanayofaa na yasiyofaa, hivyo kuyaiga.

Pamoja na utandawazi huo, ipo shida nyingine - mikakati imeelekezwa zaidi kumlinda mtoto wa kike na kumsahau kaka yake, mtoto wa kiume.

Nyumbani na shuleni, mahali kulikoaminika zaidi kuwa salama kwa ustawi wa watoto, sasa kumegeuka uwanja wa ukatili dhidi ya kundi hilo.

Imekuwa kawaida kusikia kwenye redio au kusoma gazetini na mitandaoni habari za watoto kufanyiwa ukatili wakiwa nyumbani, tena na ndugu zao wa karibu.

Pia wapo wanaotendwa unyama huo ama kunajisiwa au kulawitiwa na walimu wao wakiwa shuleni au kwenye mafunzo ya kidini huko kwenye maeneo yaliyoteuliwa kwa ajili ya kutoa elimu ya kiroho, lakini inageuzwa elimu ya 'ushetani'.

Ni miezi miwili imepita tangu Nipashe tulipoibua kashfa ya watoto kufundishwa kulawitiana shuleni kwenye baadhi ya shule mkoani Kilimanjaro.

Ni ripoti iliyoishutua serikali, ikaamua kuunda timu kupitia wizara yenye dhamana ya elimu nchini kwa lengo la kufanya uchunguzi zaidi. Moja ya hatua za awali serikali imetoa waraka, ikipiga marufuku watoto wadogo wa madarasa ya awali hadi la nne kuishi bwenini na kuzitaka shule kuwa na wasindikizaji wawili (mwanamume na mwanamke) kwa wanafunzi wanapokuwa kwenye magari ya shule.

Nipashe tunaona kuna haja jamii, hasa wazazi na walezi kuchukua hatua kwa kurudi kwenye majukumu ya msingi ya malezi ya mtoto na kuachana na dhana iliyopo sasa ya mbanano wa shughuli za kiuchumi.

Jukumu la malezi ya mtoto kuachwa kwa walimu na viongozi wa dini au kwa majirani na ndugu ni hatari kimaadili na makuzi ya mtoto. Ukatili sasa unafanywa na watu wa karibu zaidi na mtoto, yakiwamo makundi tajwa hapo juu ya walimu na ndugu anaoishi nao nyumbani.

Tumesikia na kuona matukio ya mtoto kalawitiwa na mwalimu wake, mtoto kalawitiwa na kiongozi wake wa dini, mtoto kalawitiwa na jirani yake na hata ya mtoto kalawitiwa na mjomba wake. Yote hayo yameshatokea na kuripotiwa.

Kwa kuzingatia ukweli huo, Nipashe tunaona kuna haja wazazi na walezi waondoke kwenye kivuli cha kuwa 'bize' na kazi, matukio hayo yawe filimbi vichwani mwetu kwamba tuna kitu cha ziada cha kufanya na hatua za kutakiwa kuchukua.

Shime, wazazi wanatakiwa waingie kwa miguu yote miwili kwenye usimamizi na malezi ya watoto. Dunia imeshachafuka, tuchukue hatua kuukabili mmomonyoko wa maadili kwa kuhakikisha watoto wanakua katika mienendo salama kwa ustawi wa jamii.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

## Muungwana Lazima Nilonge



# Mtindo wa wanawake kubaguana unakwamisha kufikiwa 50 kwa 50

Na Sabato Kasika

**MACH**I ni mwezi wa historia ya wanawake, hutumika kukumbuka na kuheshimu waasisi wa mabadiliko ya kundi hilo ambao walisafisha njia ya wanawake kupiga kura na kupinga ubaguzi wa kijinsia.

Wiki hii wanawake wa Tanzania waliungana na wenzao duniani kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, ikiwa na kaulimbiu 'Ubunifu na mabadiliko ya teknolojia; chachu kuleta usawa wa kijinsia'.

Kwa kuwa Machi unaitwa mwezi wa wanawake, ni vyema kujadili mambo kadhaa ambayo yanalenga kuwezesha harakati zao za kutaka 50 kwa 50 katika nafasi za uongozi, kuanzia ngazi ya chini hadi juu.

Wakati wanawake wakisaka hiyo asilimia 50 kwa 50, kumekuwapo pia dhana kwamba hawapendani, ambayo kama ina ukweli ndani yake, inaweza kukwamisha lengo la kuifikia asilimia hiyo.

Dhana hiyo ya kutopendana iliwahi kuthibitishwa na baadhi ya wanawake, katika vikao vya kufanya tathmini ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ilipoitishwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP).

Wanawake hao walidai kuwa waliwania udiwani na wengine ubunge mkoani Dar es Salaam, lakini walikatishwa tamaa na wanawake wenzao waliowaambia hawawezi kuwapigia kura kwa vile hawataki kutoa fedha.

Walidai kuwa huo mfano mdogo tu na kwamba maeneo mengi wanawake hawataki kuungana mkono badala yake wanaweka fedha mbele au kutowaamini wenzao kuwa wanaweza kuongoza.

Nikumbushe tu kwamba, mwaka ujao kutakuwa na uchaguzi wa viongozi wa serikali za mitaa, hivyo ni vyema wakati huu ambao wanawake wanaadhimisha siku yao, wakumbuke kujipanga ili kuungana mkono katika uchaguzi huo.

Kwanza nieleweke kuwa sina maana kwamba kila mwanamke anafaa kuwa kiongozi, lakini wale wenye uwezo wa kuongoza, wapewe nafasi bila kujali vyama wanavyotoka, bali kigezo kiwe ni uwezo wao.

Hilo ndilo Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akisisitiza, kwamba anateua mtu kulingana na uwezo wake wa kiuongozi, bila kujali chama anachotoka, hivyo wanawake wangechukulia uamuzi huo kwa uzito.

Lakini pia hatua ya Rais kwenda katika kongamano la maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani lililoandaliwa na Baraza la Wanawake la CHADEMA (BAWACHA), ni uthibitisho kuwa hataki kubaguana kwa itikadi za vyama.

Mwenyewe anasema habagui, wote ni wake, hivyo wanawake nao wangeiga mfano huo wa kutobaguana kwa itikadi za vyama, kwani licha ya mfumo dume kuripotiwa kuwapo, kwa kiasi fulani wanawake wanaweza kuwa wanauchangia.

Hivyo, ikumbukwe kuwa, lengo la asilimia 50 kwa 50, haliwezi kufikiwa, iwapo wanawake wataendelea kubaguana kwa itikadi za vyama au kutopendana, badala yake watajikuta wakisubiri viti maalum tu.

Ninaamini kwamba, wanawake wenye uwezo wa kuongoza katika ngazi mbalimbali za uongozi wapo, lakini kikwazo kinaweza kuwa ni kile cha wenzao kuwavunja moyo kwa kutowaunga mkono.

Kimsingi, wanawake hawana budi kubadilika na kusimama kidete kuwapigia kura wanawake wenzao wanaojitokeza kugombea nafasi za uongozi wakiwa na dhana kwamba, wanawake bila ya kuwezeshwa wanaweza.

Wapo wanawake wenye nia na uwezo wa kuongoza, ni vyema wakajaribiwa kwa kuchaguliwa katika nafasi mbalimbali, ili watetee haki za jamii, hasa ikizingatiwa kuwa wao ndio walezi wa familia.

Jambo la kuzingatia, ni wanawake kubadilika na kuondoa dhana ya kutopendana, badala yake wadumishe ushirikino na kuwa tayari kuungana mkono wakati wanapotaka kugombea nafasi kwa kushindana na wanaume.

SAFU

FIKRA MBADALA

# Viti maalum vifutwe, wanawake wana uwezo



Pascal Mayalla

**Kwa hapa nimpongeze mwanamke wa shoka kwa jina la Angelina Ngalula, ambaye ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF) na Mwenyekiti Mtendaji wa Kampuni za Bravo Logistics na Agricom Africa, ametoa kipaumbele cha wanawake majasiri au wanawake wa shoka kwenye kila eneo kwenye kampuni zake.**

SIKU ya Wanawake Duniani imepita, kwanza nitoe pongezi zangu kwa wanawake wote, bila mama hakuna binadamu, ila bila baba, binadamu yupo!

Pongezi maalum kwa mwanamke Na. 1 Tanzania, Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuliishi jina lake kwa kuleta suhuhu ya mtanziko wa kisiasa, baada ya kuruhusu mikutano ya vyama siasa nchini, siku hiyo ameshiriki kwenye tukio la chama cha upinzani, CHADEMA na kuthibitisha upinzani sio uadui.

Hiki alichokifanya Rais Samia kushiriki tukio la CHADEMA, niliwahi kuandika katika makala za nyuma kwamba 'Tunajenga nyumba moja, kwanini tugombee fito?'

Tukija kwenye Siku ya Wanawake, hakuna ubishi kuhusu uwezo wa wanawake, wanawake wana uwezo, hivyo wanachohitaji sio kuendelea kubebwa kwa nafasi za upendeleo kama viti maalum, huku kuwafanya wajione duni na kupelekea kubweteka!

Wanawake wanachohitaji ni kuwezeshwa kwa kujengewa uwezo, kupatiwa mitaji na mikopo, kuboreshewa mazingira ya biashara na kumulikiwa fursa za masoko ya bidhaa zao.

Hebu tuambizane ukweli, mwanamke amepewa ubunge wa viti maalum kwa kipindi cha miaka mitano, kwanini aendelee kuwa mbunge wa viti maalum kwa miaka mitano mingine? Ubunge wa viti maalum uwe wa kipindi kimoja cha miaka mitano tu kuwapisha wengine, baada ya miaka hiyo mitano, kama mwanamke huyo hajaweza kujenga uwezo wa kugomea jimboni, atupishe, hatufai!

Hili za viti maalum na nafasi za upendeleo kwa wanawake linawafanya wanawake wabweteke na kuendelea kusubiri kubebwa.

Kwa hapa nimpongeze mwanamke wa shoka kwa jina la Angelina Ngalula, ambaye ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF) na Mwenyekiti Mtendaji wa Kampuni za Bravo Logistics na Agricom Africa, ametoa kipaumbele cha wanawake majasiri au wanawake wa shoka kwenye kila eneo kwenye kampuni zake.

Angelina mwenyewe kwenye Siku ya Wanawake, amewapongeza wanawake wote nchini kwa siku ya wanawake na kusema kwenye biashara hakuna kazi ya wanawake wala ya wanaume, kanuni ya biashara ni moja tu - kuzalisha faida, hivyo hakuna biashara ya mwanamke au biashara ya mwanamume, biashara ni biashara tu!

Kuhusu uwezeshaji kwa wanawake, Angelina amepingana na kauli ya 'wanawake wakiwezeshwa wanaweza', anasema wanawake wana uwezo wa kuweza wenyewe na sio mpaka wawezeshwe kwa kubebwa ama upendeleo kwa sababu wanawake wana uwezo sawa na wanaume na wengine wana uwezo kuliko hata wanaume, ila ili wanawake waweze, kitu wanachohitaji sio nafasi za upendeleo au kubebwa, bali wajengewe uwezo kwa kuwezeshwa kimtaji, kujengewa mazingira bora ya biashara na kufunguliwa fursa za masoko, kitu ambacho hata wanaume wanakihitaji.

Angelina amejitolea mfano mwenyewe, kwamba japo ni mwanamke, anamiliki kampuni ya usafishaji ya malori ya masafa marefu, Bravo logistics na kampuni ya zana za kilimo ya Agricom Africa, inayoongoza kwa kuuza matrekta, zote zinasemwa ni kazi za kiume, lakini yeye ni mwanamke, ameingia huko bila kuwezeshwa kwa kubebwa, mikopo ya wanawake na ameweza, hivyo amesisitiza wanawake wanaweza kwa uwezo wao na sio kwa kubebwa.

Anamtolea mfano Rais Samia jinsi anavyoonyesha uwezo 'kuyaweza mambo mengi' ambayo huko nyuma yalishindikana.

Changamoto kubwa ni kwa wanawake wenyewe, kuziogopa baadhi ya kazi, hasa kazi zinazotumia nguvu, kwa kuziogopa na kuziona ni kazi za kiume, wakati kiukweli, hata kwa maderev wa malori, kwa malori ya kisasa, ili kuyaendesha, hauhitaji kutumia nguvu kama kubeba zege, unatakiwa kutumia akili na kujituma kwa bidii, kwa sababu kazi ya udereva inahitaji akili, umakini na kufanya kazi ya bidii na kujituma.

Nitoe pongezi zangu kwa wanawake wote wanaofanya kazi ngumu zilizokuwa zinaitwa za kiume, wakiwamo maderea, tena inatajwa kitaalamu kwamba madereva wanawake ni makini zaidi kuliko madereva wanaume. Madereva wanawake hawana zile fujo za madereva barabarani.

Nimaliizie kwa kuwapongea wanawake wote wanaofanya kazi zinaoonekana kama ni kazi za kiume, hawa ndio wanawake wa shoka! Hongera wanawake wote wa shoka!

**Paskali 0754 270403**

# Samia anastahili Tuzo ya Mo Ibrahim

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

**Kilichobainika Siku ya Wanawake Duniani Jumatano iliyopita kwenye ukumbi wa Kuringe, Moshi mkoani Kilimanjaro, Rais Samia alipokuwa mgeni rasmi kwenye kongamano la Baraza la Wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA).....**

JULAI 12, 2015, mwanachama mwandamizi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), bila shaka akiwa mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama hicho, Samia Suluhu Hassan alitokwa machozi akiwa Dodoma.

Samia alilia, si kwa uchungu, huzuni au furaha, la hasha, bali kwa mshtuko, alipofuatwa chobingo na Rais Jakaya Kikwete, aliyekuwa akikaribia kumaliza muda wake na kumpa taarifa iliyomshtua.

Rais Kikwete alimwambia: Tumeamua uwe mgombea mwenza wa urais sambamba na Dk. John Magufuli, ambaye alishatangazwa kuwa mgombea urais wa awamu ya tano kwa tiketi ya chama hicho tawala.

Samia hakuamini kama kweli alikuwa analengwa yeye, akajikuta anatokwa machozi. Rais Kikwete hakuendekeza huruma, eti kwamba amwache kwa kuwa amelia. Ndiyo kwanza akamtaka akanawe uso na aende jukwaani kutangazwa rasmi.

Alifanya hivyo kwa unyeyekevu na utiifu, kwani aliona ameaminiwa na kuheshimishwa na chama chake, akaenda kunawa uso huku moyoni akiwa bado haamini kinachotokea, huku akijiuliza; "ni mimi kweli?"

Hatimaye hilo likamalizika, akawa mgombea mwenza na kwenye uchaguzi Magufuli akashinda na kuchaguliwa kuwa Rais wa awamu ya tano, huku Samia akiwa Makamu wa Rais katika uchaguzi wa Oktoba mwaka huo.

Kutangazwa kwa Dk. Magufuli kuwa mgombea urais na Samia kuwa mgombea mwenza kulikuja miezi mitatu baada ya Aprili 2015, Dk. Magufuli kabla ya kugombea, alitoa kauli ambayo inakumbukwa sana.

Akiwa na Charles Kitwanga aliyekuja kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwenye utawala wake, wakiwa Chato kwenye mabishano kuhusu makinikia, Kitwanga alimtaka akachukue fomu kugombea urais kama alikuwa anaona mambo hayaendi.

Jibu la Magufuli likawa: "Nikiwa Rais mimi, watu watalimia meno."

Katika utawala wake wa takriban miaka saba, watu kwa kweli walishaanza kunoa meno wakalime, kutokana na aina za siasa zilizoendesha Magufuli huku akimsifia msaidizi wake Samia, kuwa mtu mwema, mchapakazi, mtiifu, mwaminifu lakini mzuri wa sura na rangi.

Machi 17, 2021, Taifa likakumbwa na mshtuko baada ya Samia kuutangazia umma, kifo cha Rais Magufuli kutokana na matatizo ya moyo. Naye baada ya siku mbili akaapishwa kuchukua nafasi hiyo na kutangazwa kuwa Rais wa awamu ya sita.

Wapo waliojiuliza anakuwaje Rais wa awamu ya sita wakati ya awamu ya tano haijamalizika! Zikatolewa sababu za kikatiba na hizi na zile.

Kilichobainika Siku ya Wanawake Duniani Jumatano iliyopita kwenye ukumbi wa Kuringe, Moshi mkoani Kilimanjaro, Rais Samia alipokuwa mgeni rasmi kwenye kongamano la Baraza la Wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA), kinathibitisha hilo, hii ni awamu nyingine kabisa.

Kilichofanyika hakikuwahi kufanyika na pengine kisingefanyika kwenye awamu iliyopita kutokana na siasa zake.

Maridhiano yanayojadiliwa baina ya Rais Samia upande mmoja na Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe upande mwingine, pamoja na vyama vingine vya siasa, ni njia pekee ya kutibu madonda yaliyosababishwa na serikali iliyopita awamu ya tano na kuunganisha Watanzania kuwa kitu kimoja.

Ile kauli ya mwanamke anaweza inajidhihirisha kwa Rais Samia. Jambo la msingi ni kumwombea mema mwaka 2025, lakini pia kumwombea apate Tuzo ya MO Ibrahim kutokana na dhamira yake chanya ya kuliunganisha Taifa.

**Alamsiki na Kazi Iendelee!**

# JKT yajipanga kuzalisha kwa tija

**Na Renatha Msungu,** KILOMBERO

SERIKALI imesema katika bajeti ya mwaka 2023/24 itaweka kipaumbele kwenye uzalishaji kwenye mashamba yanayolimwa na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), likiwamo shamba la mpunga la Mngeta ili yazalishe kwa tija na kulinufaisha taifa.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Innocent Bashungwa, wakati wa ziara ya kukagua shughuli za uzalishaji mali zinazofanywa na jeshi hilo, ikiwamo masuala ya kilimo cha mpunga kwenye shamba la mbegu la mpunga la Mngeta.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuongeza ukubwa wa shamba kutoka ekari 3,500 zinazolimwa sasa hadi kumaliza ekari zote 12,000, hatua itakayolifanya JKT ijihakikishie kujitosheleza kwa chakula na usalama wa chakula nchini.Alisema kutokana na manufaa yaliyoanza kuonekana kwenye shamba la mbegu za mpunga, serikali haina mpango wa kulirudisha mikononi mwa watu.

"Ninataka niwaambie wale wote wanaofanya ushawishi wakidhani mashamba haya tutayarudisha mikononi mwa watu, ninaomba watambue kwamba suala hilo halipo, mashamba haya yataendelea kusimamiwa na JKT kwa sababu tayari tumeshaanza kuona matokeo chanya katika kulisaidia taifa," alisema.

Alimpongeza Mkuu wa JKT, Meja Jenerali Rajabu Mabele kwa ubunifu mkubwa kwenye shamba hilo kwa kuwa wanazalisha mbegu za mpunga kwa tekonolojia ya umwagiliaji na ufugaji samaki.

Mkuu wa JKT, Meja Jenerali Mabele alimshukuru waziri kwa kutembelea miradi ya JKT na kuishukuru serikali kwa kuendelea kuongeza bajeti ya JKT kila mwaka na kuliwezesha jeshi hilo kuwekeza zaidi katika shughuli za kilimo na ufugaji hasa wa samaki.

"Fedha hizi tunazopewa ndio zinatuwezesha kufanya shughuli zote hizi, kwa mfano katika ufugaji wa samaki, hivi sasa tuna matangi 16 wakati lengo ni kuwa na matangi 27. Kwa hiyo, mpaka sasa tumeshavuka nusu ya lengo," alisema Meja Jenerali Mabele.

Awali, Mkuu wa Kikosi 837 KJ, Chita JKT, Luteni Kanali Emmanuel Kukula alieleza changamoto zinazowakabili licha ya kufanya vizuri katika shughuli za uzalishaji hasa wa mpunga.

Alisema moja ya changamoto ni uhaba wa vitendea kazi, hali inayowafanya washindwe kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

# Serikali yasaka mwarobaini wa ajali za Mlima Sekenke

**Na Elisante John,** SINGIDA

SERIKALI imeanza kutafuta ufumbuzi wa kupunguza tatizo la ajali zinazotokea mara kwa mara kwenye Mlima Sekenke ulioko Iramba mkoani hapa. Ajali hizo zimekuwa zinachangiwa na miteremko na kona kali zinazokatiza kwenye madaraja ya kina kirefu na kusababisha madereva wengi kushindwa kumudu magari yao eneo hilo la barabara kuu ya Singida-Shelui-Nzega, mkoani Tabora.

Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Singida, Msama Msama alisema hayo jana alipowasilisha taarifa ya utekelezaji miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/23 katika kikao cha 46 cha Bodi ya Barabara.

Alisema barabara hiyo ambayo imejengwa kwa kiwango cha lami mwaka 2008, ikiwa ni miaka 15 sasa, imekuwa inatumika na magari mengi yakiwamo ya uzani mkubwa, hali inayohitaji matengenezo kutokana na kuharibika.

Msama alisema hadi sasa Mhandisi Mshauri anaendelea na kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa barabara hiyo, akisimamiwa na TANROADS Makao Makuu na kazi hiyo imefikia asilimia 75.

Alimtaja Mhandisi Mshauri aliyepewa kazi hiyo kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 1.22, M/s Intercontinental Consultants and Technocrats Pvt. Ltd in JV, M/s Advanced Engineering Solution Ltd in association na M/s Intercontinental Consultants and Technocrats Co. (T) Ltd Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, James Mkwega alisema ili kumaliza tatizo la ajali eneo hilo, ni lazima jamii ishirikishwe kupata suluhisho la kudumu. "Serikali ilijenga barabara mpya ikaachana na ile ya zamani iliyokuwa inasababisha ajali, sasa tulidhani tumemaliza tatizo, lakini bado ajali zinatokea.

"Tujenge upya tena kwenye eneo hilo, kuna haja sisi Wanyiramba tukafanye jambo letu la asili pale," Mkwega alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Mwenda alisema suluhisho la ajali maeneo hayo ni kuukwepa mto kwa kupasua upya barabara pembezoni mwa mlima ili kupunguza wingi wa madaraja na kona kali.

Kuhusu kauli ya kushirikisha Wanyiramba, Mwenda alisema kwa sasa jamii hiyo imeshastaarabika na wala haijishughulishi na masuala hayo.

Mwenyekiti wa kikao ambaye ni Mkuu wa Mkoa huo, Peter Serukamba aliwataka viongozi na watendaji wa umma mkoani humo kushikamana pamoja ili kusimamia miradi badala ya kupigana majungu na kukwamisha maendeleo kwa wananchi. Alisema kazi nzuri zinazotekelezwa kwa ufanisi na baadhi ya sekta zinatakiwa kuungwa mkono badala ya kusemana na kupeana taarifa ambazo siyo sahihi.



Meneja Mwandamizi wa Benki ya Biashara ya Akiba (ACB), Magreth Mwasumbi (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, wakati wa uzinduzi wa akaunti ya Waridi, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Daktari bingwa: Watu wengi wana kisukari lakini hawajui

**Na Joseph Mwendapole**

WATANZANIA wengi wanaishi na ugonjwa wa kisukari na shinikizo la damu bila kutambua kutokana na kutokuwa na utamaduni wa kupima mara kwa mara.

Jijini Dar es Salaam juzi, Daktari Bingwa wa Hospitali ya Regency, Sudakshnina Ghosh alitoa kauli hiyo wakati wa kambi ya siku moja ya kupima magonjwa ya figo iliyofanyika kwenye Zahanati ya Regency iliyoko Mtaa wa Zanaki.

Kambi hiyo iliandaliwa na Hospitali ya Regency kwa ajili ya kuazimisha Siku ya Figo Duniani ambayo huazimishwa kila tarehe 9 Machi ya kila mwaka. "Inasikitisha sana kuona watu wengi tuliowapima tumewakuta na ugonjwa wa sukari na shinikizo la damu wakati wenyewe hawajui na wengine tumekuta shinikizo la damu likiwa juu sana," alisema.

Aliongeza kuwa walibaini watu wengi wenye uzito uliopitiliza hali ambayo alisema inaweza kuwasababishia maradhi kama shinikizo la damu na kisukari. "Uzito uliopitiliza ni tatizo ambalo linaongezeka kwa kasi sana kutokana na mtindo mbaya wa maisha wa watu kula bila kufanya mazoezi. Kuna umuhimu wa kuwaelimisha watu kuhusu ulaji bora," alisema.

Alisongeza kuwa kuna umuhimu wa kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa watu kufanya mazoezi na kufanya vipimo kuangalia kama wamepata maradhi badala ya kusubiri hali ikiwa mbaya ndipo waende hospitalini.

"Watu wanakula sana vyakula vya wanga hasa nyama choma, hivyo tuna wajibu wa kufanya kitu kuelimisha wananchi wetu kuhusu madhara ya ulaji huu usiozingatia afya na wapendelee zaidi mboga za majani," alisema

Mtendaji Mkuu wa Hospitali hiyo, Lalit Kanabar alisema wanafanya kambi kama hiyo kwa mwaka mara moja lakini kutokana na maoni ya wengi wanapanga kushirikiana na wadau wengine kuhakikisha watu wengi wananufaika na huduma hiyo kila mwaka.

"Tunafanya hivi kutekeleza maono ya Mwanzilishi wa Hospitali hii Hayati Dk. Rajni Kanabar, ambaye alitoa mchango mkubwa sana kwenye sekta ya afya hapa nchini," alisema

Robert Bona, mmoja wa waliopata huduma hiyo, alishukuru hospitali hiyo kwa kutoa huduma hiyo na kuwaomba waifanye mara kwa mara ili kuwanufaisha Watanzania wengi.

"Watanzania wenzetu wengi wana shida za kiafya lakini hawamudu kwenda kupima mara kwa mara, hivyo kambi kama hizi zikifanyika mara kwa mara zitatoa msaada mkubwa sana kwa wenzetu," alisema.

# MAISHA

MACHI 12, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 14

## Furahia juisi ya embe na hiliki

## MAISHA NI NYUMBA



Ukurasa 15




## KATUNIKA


Ukurasa 16




# Ondoa weusi mwilini

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| P | U | A | ■ | A | M | A |
| A | ■ | ■ | ■ | M | ■ | M |
| M | ■ | T | A | A | ■ | K |
| B | A | A | ■ | N | I | A |
| A | ■ | N | O | A | ■ | N |
| N | ■ | G | ■ | ■ | ■ | D |
| O | F | A | ■ | B | E | E |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


SAA, ARA, MBA, KUA, TUA, TAA, MIA, DAI, ANGAZWA, TIMBA, MBATA, KANDIKA

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI

HAYA, NI WAKATI MWINGINE TENA WA KUUNGANISHA NAMBA ILI KUPATA MCHORO KAMILI.




## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

MZUNGU mmoja alionekana kumdharau Mbongo, akamwambia waulizane maswali na akishindwa anampatia Sh. 5000 na endapo yeye atashindwa atatoa 100,000.

**Mzungu:** Nchi ipi ilishindwa kwenye vita kuu ya kwanza ya Dunia?

**Mbongo:** akashindwa akatoa 5000 kuashiria hajui.

**Mbongo:** Kitu gani kikienda juu kina miguu minne na kikirudi chini kina miguu mitatu?

**Mzungu:** akafikiria akakosa jibu akatoa 100, 000, kuashiria hajui ila akataka kujua, akauliza ni nini hicho?

**Mbongo:** Akatoa 5000 kuashiria hata yeye hajui!.

**SWALI**

Samaki aina ya Pweza ana mikia mingapi?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Misingi mibaya inavyozima ndoto za maisha ya wengi

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee kupiga darubini anga za Maisha Ndivyo Yalivyo. Leo tumulike misingi na asili vinavyorudisha watu nyuma kimaisha.

Mambo hayaendi, wanabaki wanashangaa hadi wanachukulia kuwa ni kawaida. Kumbe lipo tatizo limejificha.

Katika maisha, ipo misingi mizuri na pia mibaya. Nijikite kwenye hiyo misingi mibaya. Watu wengi sana wanajua kanuni nyingi za kufanikiwa na wanajitahidi sana. Kanuni zipo mbalimbali. Mwingine anafanya kazi kwa bidii, mwingine anaomba sana, mwingine anatoa sana sadaka. Lakini utashangaa hata baada ya kufanya hayo yote, huyu mtu hafanikiwi.

Kafanya vitu vingi sana lakini bado hafanikiwi. Matokeo anayopata na kazi aliyoifanya haviendani. Umefanya kazi kubwa, tena kwa bidii lakini matokeo ni kidogo sana. Ulichokipata siyo ulichotarajia.

Mtu amelima na kupanda mbegu lakini mavuno yamekwenda tofauti na kile alichokipanda. Hapo ndipo watu wengi huchanganyikiwa na kujiuliza, mbona nilijua ninapata mavuno mengi, mbona ibada ninahudhuria, ninatoa sadaka zote, maombi ninaomba, kuna shida gani? Nini nimekikosa, kwanini maisha yangu hayabadiliki?

Hata mwaka huu una malengo umeyaweka lakini kwanini huyafikii malengo hayo? Miezi inakwenda huu ni mwezi wa tatu kuelekea mwezi wa nne mwaka unazidi kuchanja mbuga lakini uliyoyatarajia huyaoni kama yatatimia. Kuna mahali ipo shida.

Sikiliza msomaji wangu, ukiona gari limesimama litakuwa lina mambo mawili; yaweza kuwa shida ni gari lenyewe dereva kaamua kulisimamisha au shida ni barabara gari limenasa kwenye matope.

Maana yake ni kwamba zipo sababu za nje au za ndani zinaweza kuzuia maisha ya mwanadamu kuendelea. Pia zipo sababu za ndani yako mwenyewe, ndani ya maisha yako au moyo wako mwenyewe. Inawezekana wewe ndio una shida ndio maana maisha yako hayaendi.

Lakini pengine shida siyo za kwako bali za kimazingira, zimesababishwa na waliokutangulia. Au ni misingi ya kwenu au asili ya chanzo chenu haitaki maendeleo, babu zako hawaungi mkono maendeleo. Au madhabahu za kwenu hazitaki na unapoinuka kuanza safari, ndipo zinaanza kazi.

Ukifikia hapo, chunguza misingi ya kwenu. Hatma ya mtu inayofaa ni maisha mazuri yanayosababishwa na misingi mizuri. Ukiona unaenda taratibu sana ipo shida.

Wapo watu kwa maendeleo ni kama vile mtu anabonyeza kitufe fulani fedha zinakuja. Akianza biashara asubuhi ikifika jioni ana milioni 20/- au milioni 50/-, ana faida milioni tano, milioni moja au faida 50,000/- kwa siku. Wewe unashangaa, hivi hawa wengine wanapitia wapi?

Wengine wala hawamjui Mungu lakini wanafanikiwa. Wewe unayemjua Mungu na maombi unafanya lakini ni kama hutoboi. Fahamu ipo shida mahali. Yupo mtu amesoma lakini haajiriwi. Mtu anajua vitu vizuri lakini hana fedha.

Uliyekaa naye atakuelezea habari za biashara hadi unashangaa. Yupo mtu anajuana na watu wengi hadi mawaziri lakini maisha yake hayana mwelekeo. Ukimkuta kwenye vijiwe na wenzake anavyoelezea mikakati unajiuliza ni kwanini huyu ni masikini?

Ukweli ni kwamba, hata ujuane na watu gani au uwaze kufanya biashara kubwa kiasi gani, kama misingi ya kwenu ikikataa hutaenda mahali. Ile misingi itakushikilia, itakudhoofisha. Kuna mahali fulani utakuwa umekamatwa.

Ni kwelini mcha Mungu, unahudhuria ibada, unatoa sadaka, unampenda Mungu lakini kuna nguvu fulani inakushikilia. Na Mungu hababaiki na hicho. Yupo mtu aliitwa Gideon, Mungu alimwona akajua kwanini anateseka. Ni kwa sababu kuna madhabahu ya baba yake ilimwaga damu.

Hiyo madhabahu inazuia Gideon kuendelea, na siyo kwamba Mungu alishindwa kumsaidia Gideon. Lakini Mungu akamwambia hapana, simama una uwezo nenda kwanza kabomoe ile madhabahu ya baba yako na kukatakata ile ashera (sanamu ya miungu) ndipo utapenya. Alipotimiza hilo, maisha yake hayakuwa ya kawaida tena.

Hivyo, kuna mahali unazuiliwa au ipo tabia inazuia, lipo tatizo mahali hivyo unashindwa kutoka. Lazima uharibu hicho chanzo kwa maombi makubwa ikiwa ni pamoja na kuacha tabia fulani fulani.

Ipo misingi rafiki, mingine ni kandamizi, misingi mingine ni ya dhambi, baba yako, mama yako, asili ya kwenu ni dhambi watu ni wabakaji. Mtu anajua kubaka ni jela miaka 30 lakini haachi.

**Tutaendelea wiki ijayo. Una kisa? Ujumbe 0715268581.**

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi



# Kutafuta maisha sawa, umewekeza kiasi gani kwa ajili ya afya yako?

SINA wazazi tajiri, sina baba wakubwa au wadogo ubalozini, wala bungeni. Mihangaiko yangu ya kutafuta riziki, maisha yangu ndio kama unavyojua. Usinilaumu maana kila kitu kwangu ni mimi dhidi ya dunia.

Vichocheo vya midundo ya muziki mkubwa na tangazo la afya yangu, mtaji wangu, sio kwamba sijawahi kulisikia, la hasha! Ni kwa sababu ya kutafuta maisha, ndio maana najikuta kuna mambo ya msingi kama suala la kuchunguza afya yangu litanigharimu siku za usoni, kama sitachukua hatua ya kubadili tabia na kujichunguza afya.

Ninataka kusema nini? Leo nitajikita kuzungumzia hatari ninayoiona huko mbele ya ongezeko la watu wanaopata saratani ya mlango wa kizazi.

Kwa mujibu wa Dk. Luke Nordquist wa Nebraska, Marekani, mbobezi katika saratani ya shingo ya kizazi, saratani hiyo ni mabadiliko hasi (yasiyo ya kawaida) ya chembechembe hai zilizopo kwenye shingo ya kizazi.

Kwamba, mara nyingi saratani hii ikiwa inaanza, haionyeshi dalili yoyote, hivyo mgonjwa hawezi kuchukua hatua yoyote kukabiliana na tatizo hili kwa wakati huo. Kwamba, kiasi kikubwa saratani hii husababishwa na maambukizi ya muda mrefu (persistence infection) ya virusi viitwavyo 'Human Papilloma' ambavyo huenezwa kwa njia ya kujamiiana.

Hata hivyo, utafiti wa kisayansi unaonyesha kwamba, kwa kawaida mwili una uwezo wa hudhibiti maambukizi haya yaingiapo mwilini, lakini yasipodhibitiwa kikamilifu na kuwapo mwilini kwa muda mrefu husababisha ugonjwa wa saratani ya shingo ya kizazi.

Kanzidata ya Wizara ya Afya inaonyesha kuwa Tanzania inakadiriwa kuwa na wagonjwa wapya wa saratani 42,060 kila mwaka ikiwa ni sawa na wagonjwa 76 kwa kila kundi la watu 100,000 huku nako vifo vikigota kwa watu 29,000 kwa mwaka, sawa na asilimia 68.

Siku kadhaa zilizopita, Meneja Huduma ya Kinga ya Saratani kutoka Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), Dk. Maguha Stephano alinukuliwa akisema tatizo la saratani ya mlango wa kizazi au shingo ya kizazi linaloongezeka kila mwaka, kwa kuwa kati ya wagonjwa 100 wenye saratani za aina mbalimbali wanaochunguzwa, wagonjwa 47 wanakutwa na saratani hiyo.

Kwamba kwa Tanzania, saratani ya shingo ya kizazi, ndio inaongoza kwa kuwa na wagonjwa wengi pamoja na vifo ambavyo vinatokana na ugonjwa huo.

Mabingwa wa uchunguzi wa saratani huchukua sampuli ya kinyama au majimaji/damu mwilini, baada ya kukutwa na viashiria vya saratani ya shingo ya kizazi ili kuchunguza kuwapo chembechembe za saratani (Patholojia).

Mathalani, mambo yanayotajwa na Dk. Nordquist yanayochangia kwa kiasi kikubwa kupata saratani ya shingo ya kizazi ni kufanya ngono zembe, kuwa na wapenzi wengi, kukoma siku katika umri mkubwa, utumiaji mafuta mengi katika chakula, kutokufanya mazoezi ya mara kwa mara, unene kupita kiasi, uvutaji sigara, utumiaji wa pombe kupita kiasi na kuwapo kwa historia ya saratani ya matiti katika familia.

Dalili zake za ugonjwa huu, huanza kujitokeza baada ya tatizo kuanza kukomaa, huku baadhi ya dalili zikiwa ni kutokwa na majimaji yenye harufu ukeni, kutokwa damu baada ya kujamiiana, kutokwa damu kusiko kwa kawaida (siyo damu ya hedhi), kuumwa mgongo na kiuno, kuumwa miguu na kizunguzungu na kuishiwa nguvu.

Nini kifanyike!? Kwanza kwa Watanzania ni lazima tujue kwamba saratani ya shingo ya kizazi inazuilika au kutibika kabisa, endapo itagundulika ikiwa kwenye hatua za awali. Ni muhimu kufanya uchunguzi wa afya yako kwa kadri utakavyoshauriwa na wataalamu wa afya.

Wanawake wote walio na umri kuanzia miaka 30 na kuendelea, wanatakiwa kufanya uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi. Na ukumbuke kuwa wakati wa uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi ni sasa. Usisubiri hadi uone dalili, fika kituo cha huduma za afya kwa ushauri/mwongozo zaidi.

Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Gazeti la Nipashe, Kanda ya Kaskazini.

***Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com***

***Simu ya mkononi: +255 767 535490***







Februari 26 mwaka huu ilikuwa siku ya furaha kwa Mussa Charles 'Madiaba' na mkewe Kataka Mashauri, baada ya kufunga ndoa katika Kanisa Katoliki kijijini Suguti, Musoma Vijijini mkoani Mara.





## MITINDO

# VIJANA HAPA VIPI?



TUNAENDELEA kuwapa njia mbalimbali za kuwapa muonekano bomba wanaume, hasa wale wanaohitaji kuvaa vizuri.

Unaweza kutoka tofauti kama utakua mbunifu wa mitindo, kwa wajanja vazi la Sweta lenye shingo ndefu ni moja ya chaguo lao la kwanza.

Kihistoria inaonyesha Sweta ya shingo ndefu, ilibuniwa kwa ajili ya kupambana na hali ya baridi, lakini sasa limeboreshwa na kutumiwa nyakati zote.

**UMARIDADI**

Sweta la shingo ndefu limekuwa maarufu na linapendwa wakati wote na vijana.

Hata hivyo, wengine wanaweza kununua endapo watahitaji kupata mwonekano tofauti. Nguo hizi kwa kawaida hutengenezwa kwa pamba na sufu.

**UTACHAGUA VIPI?**

Endapo unapenda kuvaa nguo ya aina hii, unatakiwa kuhakikisha unaangalia mitindo na ubora wake.

Chagua rangi nzuri na ukubwa unaolingana na mwili wako kwa sababu ukikosea unaweza kuondoa uhalisia wako.


Angalia shingo ya sweta kama inavutika kwa sababu inatakiwa kutanuka na kurudi pale unapoivaa.





URE MBO

Na Mary Geofrey



# Ondoa weusi mwilini

WEUSI kwenye ngozi ya magoti na kwenye viwiko vya mikono ni jambo linalo wakera wanawake wengi.

Hata hivyo, tatizo hili litaondoka kama utang'arisha ngozi ya magoti na nyuma ya mikono kwa kutumia vitu mbalimbali vya asili.

Mafuta ya mzeituni, sukari

Chukua vijiko vikubwa vinne vya mafuta ya mzeituni kisha changanya na kijiko kikubwa cha sukari kimoja.

Tumia kwa kupaka kama kilainishi kwenye magoti au nyuma ya mikono, kisha tumia mikono kuchua kwa muda wa dakika tatu mpaka tano. Kaa kwa muda wa dakika thelathini kisha nawa kwa maji ya uvugu vugu.

Juisi ya Alovera

Paka fresh juice ya alovera kwenye ngozi ya goti halafu iache kwa muda wa nusu saa kisha tumia kusafisha kwa maji ya moto au vuguvugu.



Binzari manjano, asali, maziwa

Chukua binzari ya manjano kijiko kimoja kikubwa, asali vijiko vinne vya chakula na maziwa fresh vijiko vinne vikubwa vya chakula.

Vichanganye vyote kwa pamoja kisha tumia kupaka kwenye magoti, halafu iache kwa muda wa dakika thelathini na nawa kwa maji ya uvuguvugu.

Ndimu

Kata kipande cha ndimu kisha tumia kusugua kwenye magoti. Goti moja kwa kila kipande. Sugua kwa muda wa dakika tatu hadi tano kisha kaa nayo kwa muda wa saa moja.

Utafanya hivyo mara mbili kwa siku asubuhi na jioni kwa muda wa siku thelathini.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Furahia juisi ya embe na hiliki



MSIMU kama huu, matunda ni mengi hasa embe hivyo ni rahisi kutengeneza juisi na kufurahia na familia yako.

Leo tutaelekezana namna ya kutengeneza juisi ya embe iliyotiwa hiliki na ufurahie ladha nzuri.

**Namna ya kuandaa**

Chemsha maji ya kutosha lita mbili hadi tano kulingana na wingi wa matunda uliyonayo na unataka juisi uzito gani.

Chukua matunda yako na uyaoshe vizuri kwa kutumia maji ya vuguvugu yaliyowekwa chumvi kiasi ili kuua vijidudu.

Menya matunda yako bila kujikata vidole na katakata matunda vipande vidogo ili kuiwezesha blenda yako kusaga matunda kwa urahisi.

Chukua matunda, hiliki na tangawizi kisha weka katika blenda na anza kusaga.

Unaweza kuongeza maji yaliyochemshwa wakati wa kusaga ili kupata mchanganyiko wa wastani usio mzito sana.


Chukua maji yaliyochemshwa changanya na uji wa matunda kwa kiasi kulingana na wingi wa matunda na kisha koroga.

Chuja mchanganyiko wako huo na chukua sukari na uitie kisha koroga vizuri.

Chukua chombo safi maalum cha kuwekea juisi na anza kuitia kwenye vyombo na uweke kwenye friji ipate baridi tayari kwa kunywa.

MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Hivi ndivyo unavyoweza kutumia kona ya chumbani

KILA kona ya chumba iliyo tupu ni fursa yako kubuni namna ya kuipendezesha.

Wakati unaipendezesha, una fursa ya kuitumia pia hata kama awali ilikuwa inaonekana haiwezi kufaa kwa matumizi.

Zipo njia nyingi za namna ya kubuni kutengeneza kona yako ikapendeza na hata kupendezesha nyumba yako pia.

Njia mojawapo unaweza kuamua ukaitumia kama shelfu ya kuhifazia vitabu vyako kwa kuitengeneza kufuatisha muundo wa kona.

Hii ni moja ya njia nzuri kufanya isiyokuwa na kitu itumike na shelfu zinaweza kutengenezwa kwenda juu karibu na dari kulingana na mahitaji na ukubwa wa kona ya nyumba yako.

Mbali na shelfu za vitabu, pia unaweza kutengeneza kona yako kwa ajili ya kuweka mapambo madogo.

Pia kona inatumika kutengeneza sehemu ya kufanyia shughuli mbalimbali za kiofisi au kusomea.

Kumbuka sehemu ya kona ikitengenezwa vizuri ni nzuri zaidi na hutuliza akili hususani kwa wanaosoma.

Pia unaweza ukaitumia kona kama sehemu ya kutundika picha za familia.

Huhitaji ukuta mkubwa kwa ajili ya kusambaza picha za familia yako badala yake tumia kona hiyo kuongeza mvuto na pia usiweke nyingi zikakuharibia mvuto.

Pia kuweka ua la mmea wa kuoteshwa endapo hutataka kuweka shelfu au sanaa zozote na itasaidia kuingiza uoto asili ndani ya nyumba kwa sababu matawi yake yatatosha kuijaza kona yenyewe.

Kwenye chumba, kona hiyo unaweza kuitengeneza vizuri kama sehemu ya kutundikia nguo hasa kwenye chumba cha kunyooshea au kinachotumika kwa ajili ya kulala.

Hata kwenye chumba cha wageni ambacho mara nyingi huwa sio kikubwa, unaweza kuitumia kupachika mbao nyembamba zinazoweza kukutanisha pande zote mbili za ukuta na hapo ukatundika nguo zako na zikakaa katika mwonekano mzuri.

Na kwa wenye sebule au vyumba vyenye nafasi ndogo, kona inafaa pia kuweka sofa hasa la duara lenye vipande viwili ambavyo vinaunganika.

Pia unaweza kupendezesha kona yako kwa kuweka vinyago ambavyo navyo lazima uweke juu ya meza ndogo au ukapatengenezea kabati au meza ya miguu mitatu.

Ni vizuri zaidi pia ukimtumia fundi kukufanya 'dizaini' ya namna ya kutumia kona yako kulingana na kitu utakachoona kitaipendezesha zaidi.

## Ijue 'console' na matumizi yake ndani ya nyumba

**Na Restuta James**

KUNA meza hii ambayo watu wengi hawaipi uzito wa kuwepo ndani. Wengi wanazingatia kupata meza ya kulia chakula pamoja na ile ya kahawa (coffee table), ambayo mara nyingi huiweka sebuleni.

Leo ninakuletea meza ya 'console' ambayo ina umuhimu wa kipekee ndani ya nyumba. Wataalam wa mapambo wanaieleza kama meza muhimu ya kuweka vitu 'adimu' na muhimu.

Wanaeleza kuwa ni meza inayoweza kutumika kuweka chetezo cha udi kwa wale wanaopenda marashi hayo na pia inafaa kwa matumizi ya mishumaa.

Hapa ndipo unapoweza kuona umuhimu wake. Wanaeleza kuwa si kila mahali chetezo inaweza kuwekwa; jambo ambalo halina ubishi.

Kwa wapenzi wa mishumaa yenye harufu nzuri, meza hii inawahusu sana. Wataalamu wanatukumbusha kwamba si kila mahali panafaa kuweka mishumaa hiyo.

Wanaeleza kuwa inaweza kuwekwa kwenye korido karibu kabisa na sebuleni au nyuma ya sofa kubwa kulingana na mpangilio wa sebule yako.

Kadhalika, inaweza kuwekwa karibu na sehemu ya kunawia mikono mnapolia chakula.

Kwa kuwa ina matumizi maalum ya kuweka manukato, haipaswi kuwa mbali sana na maeneo hayo.

Hata hivyo, wanashauri kwamba meza hii inapaswa kuwa ndogo na ndefu wastani na pia inakishiwe kwa vitu vichache.

Inaweza kuwa na droo na inapendeza zaidi kama itakaa kwenye ukuta wenye kioo.

Wataalam wanatahadharisha kwamba kamwe meza hii haipaswi kuwa stoo ya kuhifadhia vitu. Isitumike kuweka madaftari au vitabu vya watoto.

Kama ni lazima sana basi unaweza kuweka jarida maridhawa unaloweza kupepesa macho pindi unawasha mshumaa au udi wako na si vinginevyo.


Pia inaweza kutumika kuweka picha nzuri moja tu ya familia au ya mtu mahsusi ili unapowasha mshumaa upate tabasamu. Pia unaweza kuweka ua dogo la asili au la kutengeneza.

Meza hii inatajwa kama sehemu inayoweza kumtambulisha mwenye nyumba kwa mgeni.



Kwa mujibu wa wataalam hao ni kwamba hii ni meza inayoeleza hisia za mwenye nyumba.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
HA HA HAAAA HAAW!
MFUPI KAMA JIWE!
MPIGA MIZINGA YA BIA
JUKWAANI
?
MIJINI
HE!
MZEE SIKU HIZI NAJISHANGAA KILA NIKILALA NAOTA NIMEKUFA LAKINI NAHEMA!
KALETE FEDHA ULIZONAZO BENKI TUZITAMBIKIE, TUONDOE KUHEMA
HUU MZIKI ULIUSIKIA KABLA HUJAPANDA, NA UNGEONA UNAWEZA KUKUKERA USINGE-PANDA!
MAJIBU YAKO YANAASHIRIA KAZI HII, HAIKUFAI
MAJIBU KAMA HAYO AKAMJIBU MKEWE NYUMBANI
MZEE JIHE-SHIMU, KWANI MKEWE KAM-TUMA?
DEREVA HAYO SIO MAJIBU
KUBWA ZIMA UNAJILIZA KAMA UMEFIWA!"
WE UNADHANI MSIBA MPAKA AFE MTU! HATA KUONDOKEWA NA "DILI" PIA MSIBA
NAKUHAKIKISHIA KUWA NAKUUZIA SIMU AMBAYO "INAWAKA" HAIJAZIMA
KWA HIYO NIKIINUNUA KUZIMA MPAKA NIITE "FAYA?"
*KINYUNYIZO CHA LEO...
DEKA KWENU, DEKA JELA UONE...

## Iran, Saudi Arabia zapongezwa kurudisha uhusiano wa kibalozi

**RIADH,** Saudi Arabia

NCHI za Marekani na Ufaransa zimekaribisha hatua ya Iran na Saudi Arabia kutangaza kurejesha uhusiano wa kidiplomasia.

Katika taarifa ya pande tatu iliyotolewa siku ya Ijumaa, Iran yenye Waislamu wengi wa madhehebu ya Kishia na Saudi Arabia yenye Waislamu wengi wa madhehebu ya Kisunni, HYPERLINK "https://www.dw.com/sw/iran-na-saudi-arabia-zarejesha-uhusiano-wa-kidiplomasia/a-64949087" zilitangaza kuwa zitafungua tena balozi ndani ya miezi miwili.

Pia zilitangaza kutekeleza mikataba ya usalama na ushirikiano wa kiuchumi iliyotiwa saini zaidi ya miaka 20 iliyopita.

Ikulu ya Marekani White House, imepongeza makubaliano hayo, na kuongeza kuwa inasubiri kuona iwapo Wairani watatimiza wajibu wao.

Ufaransa pia imepongeza hatua hiyo, ikisema inaunga mkono mazungumzo, lakini imeitaka Iran kuachana na vitendo vyake vya kuvuruga utulivu.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres, amekaribisha tangazo hilo na kusema bado yuko tayari kutumia ofisi yake kuendeleza mazungumzo ya kikanda.

Mwanadiplomasia mkuu wa Saudi Arabia, Mwanamfalme Faisal bin Farhan Al Saud, alisema makubaliano hayo yanatokana na dhamira ya serikali ya Kifalme ya kutaka suluhu za kisiasa na mazungumzo.

Naye waziri wa mambo ya nje wa Iran, Hossein Amir-Abdollahian, alisifu hatua hiyo akisema nchi yake itatayarisha kikamilifu mipango mingine ya kikanda. Kurejea kwa uhusiano wa kawaida kati ya nchi hizo mbili kunatoa utulivu wa kikanda na ulimwengu wa Kiislamu.

Saudi Arabia ilikata uhusiano na Iran baada ya waandamanaji wa Iran kushambulia ofisi za kidiplomasia za Saudia mwaka 2016, kufuatia mauaji ya mhubiri wa Kishia mwenye ushawishi Nimr al-Nimr.

Tangazo la juzi linafuatia siku tano za mazungumzo ambayo hayakutangazwa hapo awali yatakayofanyika nchini China, Iraq na Oman.

Mshikamano kati ya Saudi Arabia, msafirishaji mkubwa wa mafuta duniani, na Iran ambayo inavutana na nchi za Magharibi kuhusu mpango wake wa nyuklia, unaweza kurekebisha uhusiano katika kanda ya Mashariki na Kati ambayo inakabiliwa na misukosuko kwa miongo kadhaa.

**DW**

# Kimbunga Freddy chaleta hofu Msumbuji

**MAPUTO,** Msumbiji

KIMBUNGA Freddy kinatarajiwa kutua nchini Msumbiji kwa mara ya pili baada ya kusababisha vifo vya takriban watu 27 kilipotua nchini humo na Madagascar, kwa mara ya kwanza mwezi uliopita.

Wanasayansi wanasema mabadiliko ya tabia nchi yanasababisha vimbunga kuwa na mvua kubwa na upepo mkali zaidi.

Raia nchini Msumbiji wanajitayarisha kwa mvua kubwa wakati kimbunga hicho kikitarajiwa kutua kwa mara ya pili nchini humo katika tukio ambalo si la kawaida kwa mujibu wa wataalamu.

Maelfu ya watu tayari wameachwa bila ya makazi. Huenda zaidi ya watu nusu milioni wakawa katika hatari ya kukumbwa na janga la kibinadamu wakati kimbunga hicho kikipiga nchi hiyo.

Idara ya hali ya hewa duniani (WMO) ilisema kimbunga Freddy kinaaminika kuelekea kuwa kimbunga cha muda mrefu. Rekodi iliyoko sasa ya muda wa kudumu kimbunga ni siku 31.

Kilianza kutoka pwani ya Australia kaskazini mapema Februari na baadaye kusafiri kuelekea maelfu ya kilomita katika bahari ya Hindi kutoka mashariki hadi magharibi, na kuviathiri visiwa vya Mauritius na Reunion, kabla ya kutua Madagascar wiki mbili baadaye hatimaye kuelekea Msumbiji.

Idara hiyo ya hali ya hewa duniani ilisema ni nadra kwa kimbunga kuzunguka na kurudi tena na wamekitaja kama tukio la kushangaza.

**BBC**




Kampuni ya Czech inayozalisha silaha ikionyesha moja ya kifaru chenye uwezo wa kurusha roketi za Himars. Imeelezwa tangu uvamizi wa Russia nchini Ukraine, kampuni hiyo imepata faida kubwa kutokana na mauzo ya silaha. **PICHA: AFP**

# Kesi ya Kabuga yasimamishwa ICC

**THE HAGUE,** Uholanzi

KESI ya Felicien Kabuga, ambaye anashukiwa kufadhili mauaji ya halaiki ya Rwanda mwaka 1994, imesitishwa katika mahakama ya Kimataifa (ICC) iliyoko The Hague, nchini Uholanzi.

Felicien Kabuga (90), alikuwa akikabiliwa na kesi hiyo baada ya kukwepa kukamatwa kwa miaka 26, lakini mawakili wake walisema ana shida ya akili na hastahili kushtakiwa.

Kesi hiyo imesitishwa kupisha mtuhumiwa huyo kupimwa afya yake.

Inadaiwa Kabuga alifadhili wanamgambo wa kabila la Wahutu ambao waliwachinja Watutsi wapatao 800,000 na Wahutu wenye msimamo wa wastani.

Mauaji hayo yalifanyika kwa muda wa siku 100 pekee. Inadaiwa kuwa alitumia utajiri wake alioupata katika biashara ya chai miaka ya 1970, kununua mapanga na kuwapa wauaji.

Mfanyabiashara huyo tajiri pia anatuhumiwa kutumia kituo chake cha redio kuwahimiza Wahutu kuwaua Watutsi, na hivyo kuchochea mauaji ya halaiki kwa kutangaza matamshi ya uchochezi ya chuki.

Hata hivyo, Kabuga alikana mashtaka yote.

Kabuga alikamatwa mwaka wa 2020 baada ya kushindwa kukaa mafichoni miongo kadhaa.

Wachunguzi wa Ufaransa walimtafuta hadi kwenye ghorofa moja huko Paris ambako alikuwa akiishi akiwa na utambulisho wa uongo.

Manusura wa mauaji ya halaiki hapo awali walielezea wasiwasi wao kwamba haki huenda isitendeke ikiwa Kabuga atafariki bila kuhukumiwa katika mahakama ya ICC.

**BBC**

SAFU/MAKALA

SIKU YA WANAWAKE DUNIANI

# Uthubutu, uwezeshaji kielimu unavyopaisha wanawake mgodini

**Na Mwandishi Wetu**

MTU anapojitambulisha kuwa anafanya kazi mgodini, watu wengi hudhani kuwa kazi zilizopo ni kuingia chini ya ardhi kutafuta madini. Dhana hiyo imesababisha baadhi ya watu kuamini kuwa kazi yoyote mgodini ni ya wanaume, lakini dhana hiyo ni tofauti kwa Neema Mwidibo ambaye amefanya kazi katika sekta ya madini kwa miaka 20 sasa.

Neema, mama wa watoto wanne, alijiunga na Kampuni ya Geita Gold Mining Limited mwaka 2005 na kuanza kufanya kazi kama mpokezi wa taarifa kupitia redio na kuingiza data akiwa na elimu ya kidato cha sita pekee.

Hivi sasa mama huyu ni Ofisa Mwandamizi Idara ya Ununuzi, anayeelezea historia yake mpaka kufikia mafanikio hayo, akitamka: "Nilizaliwa katika Kijiji cha Nyarugusu mjini Geita. Baada ya kumaliza elimu ya kidato cha sita hapa Geita, nilipata hamasa ya kufanya kazi mgodini baada ya kuona ndugu zangu walioajiriwa na GGML wakifanikiwa kimaendeleo."

Anasema alipojaribu kutuma maombi ya kazi ndani ya mgodi, alipata kazi kwa mkandarasi mmoja aliyekuwa amepewa zabuni na GGML, kisha baada ya miaka miwili ndipo akahamia GGML kama mpokeaji wa taarifa kwa njia ya redio na mhifadhi data.

Kwa kuwa elimu yake ilikuwa ndogo, alipata hamasa ya kujiendeleza kielimu, hivyo akawa anaweka akiba ya fedha ili kutimiza lengo hilo.

Taratibu alijiunga na masomo kwa njia ya mtandao katika Chuo cha Cambridge cha Uingereza na kufanikiwa kupata stashahada ya ununuzi iliyomwezesha kuhamia katika Idara ya Ununuzi ya GGML.

Anasema baada ya mwaka mmoja na miezi kadhaa, aliamua kurudi tena masomoni, akichukua shahada ya masuala ya ununuzi, safari hii akilazimika kuacha kazi ili kupata muda wa kutosha katika masomo yake.

Anasema kuwa baada ya kuhitimu, alirejea GGML akapokewa na kupatiwa nafasi ya juu zaidi kama Ofisa Ununuzi Mwandamizi kwenye Kitengo hicho cha Ununuzi.

"GGML imekuwa maisha yangu, wote tunafahamu umuhimu wa ajira, kuwa mwajiriwa imenisaidia kuendesha maisha yangu. Ninaweza kuhudumia familia na kufanya biashara mbalimbali," anasema na kubainisha kuwa pia wanapewa mafunzo maalum na mgodi ya kuwajenga uwezo wanawake kushika nyadhifa za juu za uongozi.

"Katika mafunzo hayo nilikutana na wanawake wenye nafasi kubwa kwenye kampuni tofauti tofauti, hali hiyo ilinifanya niamini kwamba inawezekana na mimi kama mwanamke kufikia ngazi za juu. Nikiwa katika mafunzo yale nilijifunza mambo mbalimbali ya uongozi na programu nyingine tofauti tofauti," anasema.

Anabainisha kuwa ndani ya GGML, wanawake wanapewa kipaumbele kikubwa katika fursa mbalimbali kuanzia, mafunzo ndani ya kampuni, elimu na hata ajira.

Ni kauli inayoungwa mkono na Lina Sitta, Ofisa Mwandamizi wa Mafunzo kwenye Idara ya Uchenjuaji Dhahabu ya GGML, anayebainisha safari yake aliianza mwaka 2003 akiwa mwalimu msaidizi kwenye shule ya watoto ya International School of Geita inayomilikiwa na GGML ambako alifanya kwa muda wa miaka saba kisha akahamishiwa upande wa shule ya msingi ambako alifanya kwa miaka minne.

Baadaye alipandishwa cheo na kuwa Ofisa Usalama na Mafunzo ambako alifanya kwa miaka minne kisha akawa Ofisa Mwandamizi Usalama na Mafunzo.

Lina anasema mafanikio hayo ameyapata kutokana na fursa anazopewa ndani ya GGML kutoka nafasi moja kwenda nyingine.

"Mafanikio yalikuja hasa kwa kufanya kazi kwa bidii. Mimi ni mwalimu lakini nilitumia zile faida nilizonazo wakaona ninaweza kupanda na kufanya kazi yenye matunda kwa kampuni," anasema.

Anasema GGML imekuwa mstari wa mbele kuunga mkono juhudi za wanawake kwa kuanzisha programu mbalimbli ambazo zinaweza kuwainua na kuwaendeleza ili wazitambue haki zao.

**SIKU YA WANAWAKE**

Akizungumzia siku ya wanawake duniani ambayo huadhimishwa kila mwaka Machi 8, Lina anatoa wito kwa jamii kumwandaa mtoto wa kike kuanzia ngazi ya familia ili awe na ujasiri, kujitambua na kujiamini kuwa anaweza kuwa kiongozi.

"Ni muhimu kuwaandaa watoto wa kike. Majukumu yao sio kuosha vyombo, kubeba mimba na kujifungua, kuna mengine zaidi. Lakini pia jamii inatakiwa kutengeneza ushirikiano ili mtu aendane na mazingira ambayo yatamfikisha mbali zaidi kimaisha.

"Kampuni zenye wafanyakazi wa kike, ziweke programu mahsusi ambazo zitafanyiwa tathmini kila mara kwamba inapiga hatua kwa kiasi gani kusaidia wanawake hao kukua," anashauri.

Dk. Subira Joseph anayefanya kazi GGML kwa zaidi ya miaka 10 sasa, anasema kampuni hiyo imempa fursa mbalimbali za kukua kielimu na kitaaluma.

"Ninaweza kukabiliana na majukumu mbalimbali kama vile kuongoza idara yangu, ni dhahiri kuwa kupata mafunzo yale yanayotolewa na mgodi, yamenisaidia sana," anasema.

Anakumbusha kuwa wakati anaingia GGML, hapakuwa na madaktari wa kike, hivyo baadhi ya wafanyakazi wanawake walipata shida kwenda kujieleza kwa madaktari wa kiume ili kupata matibabu, hivyo kuwapo mchanganyiko wa wafanyakazi wanawake na wa kiume kumeongeza ufanisi ndani ya kampuni.

"Ushauri wangu kwa wanawake wengine ni kwamba tusiogope kujiunga na sekta hii ya madini kwani ni sekta kama zilivyo sekta nyingine, hivyo kunapotokea fursa ya kazi, tuombe na kuja kufanya kazi kwani hakuna chochote cha ajabu na sekta nyingine," anasema.

Josephine Kimambo aliyeajiriwa GGML baada ya kupata mafunzo kwa vitendo mgodini huko alipohitimu masomo ya chuo kikuu, anasema kilichomvutia kufanya kazi kwenye sekta ya madini, ni fursa iliyoko huko ya kujifunza mambo mengi ndani ya kipindi kifupi.

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

## *Mwanamke aliyetaka kuvunja ndoa ya shoga 'ake, kisa uzuri wa tausi*



**Na Adam Fungamwango**

MAPENZI ni ridhaa ya watu wawili tu. Wanakutana wenyewe sehemu ambayo walijijua wenyewe, wakaongea wanayoongea, wakaelewana. Kila mtu akamuelewa mwenzake wakapendana. Wanaweza wakaendelea na mapenzi yao, wakati mwingine kufika hadi kuoana.

Kama kila mmoja akinitumia meseji atasema siku ya kwanza alipokutana na mwenzi wake, kila mtu atashangaa. Na itakuwa burudani tosha kwenye safu hii.

Mapenzi ni kitu cha ajabu sana. Hivi sasa watu wapo kwenye ndoa, lakini ukiwauliza walionana wapi, unaweza kusikia mume akisema,"nilikwenda kwa dada yangu, akaja binti mmoja kuomba maji ya baridi, nikamuuliza huyu hivi, akanijibu ni binti wa jirani hapo, nikawa nimempenda, ndiyo unaona hadi leo mke wangu."

Mke naye anaweza kukwambia alikwenda kwa mama yake mdogo, huko akakutana na kijana ambaye leo hii ndiye mumewe.

Wengine wanakutana kwenye daladala, mabasi ya kusafiri mikoani, ndani ya treni.

Kuna ndugu yangu mmoja yeye alipata mke kwenye stesheni ya Salanda. Treni ilisimama hapo kwa muda mrefu kwa ajili ya mambo yetu yale ya kula wali au ugali kwa kuku. Mmoja wa waliokuwa wanamsaidia mama mmoja kuuza ni msichana mmoja ambaye yeye kwa macho yake alionekana kumpenda. Lakini kwa wakati huo asingeweza kufanya chochote. Treni ilisimama kwa muda tu, walikuwa wanasubiri honi tu waondoke.

Alichokifanya ni kumwita akawa anamtuma kaniletee chumvi, pilipili, huku akimuuliza jina, na akamwambia yeye ni mgeni pale ameshuka na treni, lakini alikuwa na maongezi marefu na yeye, hivyo anaomba namba yake.

Binti akamjibu yeye hana simu, ila anatumia ya shangazi yake. Ndugu yangu akaandika namba yake ya simu, na kumwambia, kesho yake ampigie au ambipu ili afanye utaratibu wa kumtumia pesa ya kununulia simu.

Honi ikalia, watu wakaingia kwenye treni, ndugu yake na binti yule wakaagana. Na kweli kesho yake binti alimbipu kwa kutumia simu ya rafiki yake. Wakaongea mengi, lakini kilichofanyika ni kwamba binti alitumiwa pesa ya kununulia simu ili wapate urahisi wa kuongea. Binti akanunua simu, sasa kukawa na mawasiliano ya moja kwa moja baina yao. Kilichoendelea ni kwamba baadaye binti alitumia pesa ya nauli kwenda Dar es Salaam kumfuata ndugu yangu ambaye alimwambia ametokea kumpenda.

Leo hii ni mke na mume. Hakuna sehemu sahihi ambayo imewekwa kuwa mchumba atapatikana. Rafiki yangu mmoja alimpata mchumba hospitali. Tulikuwa tunakwenda kumuangalia rafiki yetu mwingine aliyekuwa amelazwa. Msichana huyo naye alikuwa akija na ndugu zake kumwangalia mjomba wake. Macho yao yakagongana. Wakaelewana, leo ni mke wa mume.

Nakumbuka kwenye msiba wa baba yangu mzazi, mmoja wa jamaa zangu alipata mchumba, leo hii ni mkewe na wana watoto wawili.Stori hizi nimezieleza kutaka kuonyesha kuwa wengi hawajui mwanzo wa mapenzi ya watu. Lakini baada ya hapo, wanapopusa sasa fulani na fulani ni wapenzi, wanakuwa kimbelembele utafikiri wao ndiyo wamewaunganisha.

Kitu kidogo tu, basi umbea utapelekwa huku na mwingine utakwenda kule, ili mradi tu kuwagombanisha. Kwa haraka haraka unaweza kudhani kwamba wanawapenda na hawataki mapenzi na ndoa yao isambaratike, lakini kumbe ni uongo na uzushi mtupu.

Rai tu kwa wanandoa na ambao wako kwenye uchumba au mapenzi, wasiwe wepesi wa kusikiliza watu wa pembeni. Kama kuna kitu umekisikia, chunguza kwanza mwanzo wake, sababu na ukweli kuhusu jambo hilo, kuliko kukurupuka na kukasirika.

Unaweza ukavunja uchumba, mpenzi au ndoa, halafu baadaye ukaja kuta kumbe si kweli, halafu ukashindwa kulirudisha ikabaki kilio na kusaga meno.

Zahir Ally Zorro, akiwa na JKT Mafinga, maarufu kama 'Kimulimuli', alitunga wimbo uitwao 'Uzuri wa Tausi.' Unamhusu mmbea mmoja aliyemfuata dada aliyeolewa na kumjana maneno ya uchochezi ili amchukie mumewe.

Akamwambia kama mumewe ni mwanamuziki mbona hajawahi kusikia amemtungia wimbo na kumuimba? Kila siku anawataja wanawake wengine? Hao wanawake wengine anaowaimba si bure huenda ni mabibi zake. Mke wa huyu mwanamuziki ni mmoja kati ya wanawake wa shoka na mfano wa kuigwa. Badala ya kumkasirikia mumewe na kuanzisha ugomvi bila kufikiri, akaona huu ni uchanganishi na nia ni kuvunja ndoa yake.

Akaamua amfuate huko huko nyumbani kwake, akampasha mbele ya watu. Haya ndiyo mashairi wa wimbo huu, mke alipomchamba mfitini.

"Haya ni maneno ya ugombanishi, ni maneno ya uvunja nyumba, aa shoga yangu unataka kuniachanisha na mume wangu, nakupasha nimeshtuka.

Shoga leo nisikilize, shoga leo nikupashe na urafiki wetu utakwisha leo, nakuona una nia mbaya, uje uniachishe kwa mume wangu, ooo shoga yangu eee.

Shoga wewe ulisema maneno mengi, lakini haya ya leo nashindwa kuvumilia, naona mwisho nitakuja achwa, uje kunicheka.

Shoga ni wewe uliyesema, kwa kuwa mume wangu ni mwanamuziki, kama kweli ananipenda, angeniimba kwenye nyimbo zake, na kunifananisha na ndege tausi oo shoga yangu ee.

Shoga sasa nitakupasha, nywele za tausi hazihitaji kitana, miguu ya tausi haihitaji viatu, macho ya tausi hayapakwi wanja, mimi ni binadamu tausi ni ndege, uzuri wa tausi nitaupata wapi, tausi mwenye rangi eee." Habari hizi zinamfikia mumewe. Akampongeza mkewe kwa alichofanya kwa mustakabali wa ndoa yao, akamwambia mkewe maneno yafuatayo ambayo nayo yapo kwenye wimbo huo huo.

"Umempasha vya kutosha mama ooo, atazame ustaarabu wa kwake lololo, asifuate mambo yasiyomuhusu, atazame ustarabu wa kwake lololo. Na kama ni kukusifu wewe mama watoto wangu, jukumu hilo ni langu mimi mumeo. na sasa naamua.

Mama watoto pasenti miamoja, kwa ukarimu kwa wageni wetu nyumbani mama ooo, mama watoto pasenti miamoja, kwa kuitunza familia yetu na watoto mama ooo, mama watoto pasenti miamoja, pamoja na kuwa na heshima kwa pande zote mbili, mama ooo."

Narudia tena, mapenzi ni ya watu wawili tu. Akiingia wa tatu ni mvurugaji tu.

Je wewe wakwako ulimpata vipi?


**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

MIEZI miwili tu baada ya ndoa, Husna anapigiwa simu ya mtu asiyemfahamu. Haikuwa simu ya heri. Ni simu ya mtu anayeonekana amedhamiria. Amedhamiria kufanya kitu alichokikusudia. Kwenye maisha ya ndoa aliambiwa yatakuwa ya shida na raha, lakini kwake haikuwa mapema kiasi hicho. Alihisi sasa hakuingia kwenye ndoa aliyoikusudia bali ni ndoa ndoana.Ni nani aliyempigia simu Husna? Alitaka nini? Lengo lake hasa ni nini? Ni kweli alichokusudia mpiga simu ndicho alichokihitaji ili kuvuruga ndoa hiyo? Nenda hatua moja moja kwa kusoma kila nakala ya toleo la Nipashe ili upate ukweli mzima wa kisa hiki cha utata, kusisimua, kusikitisha na chenye mafunzo makubwa kwa jamii na wanandoa wote.

# Simu ya sumu-1

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**




ENHEEE ndiyo wewe nilikuwa nakutaka shoga angu. Nilikuwa nakutafuta haswa. Mwanamke usiyekuwa na haya, usiojua kupendeza sketi, blauzi, dela, suruali wala kijora. Bibi wewe hupendezi sokoni wala 'super market,' mwanamke usioujua wanja, shedo wala lipstick, saluni wewe kwako kituo cha polisi...."

"Samahani kwani wewe nani mwenzangu?"

"Tulia hivyo hivyo wewe kama unanyolewa, utanieleza nini wewe, yaani umeing'ang'ania ndoa hadi umeipata, sasa sikiliza huwezi kukaa kwa raha na huyo mwanaume wakati mimi nipo hai. Mimi ndiyo ilikuwa niolewe na huyo mwanaume, unamfanyia dawa, unamlisha limbwata, kaniacha, kaja kukuoa, sasa mimi na wewe, nakula na wewe sahani moja na hii ndoa haipo tena miezi mitatu nahakikisha inasambaratika..."

"Dada kwani wewe ni nani, mbona sikuelewi?"

"Huna haja ya kunijua na wala sina haja ya kukutambulisha kikaragosi kama wewe mwanamke usiojua kumlea bwana, mwanamke usiyojua kumlea mwanaume, usiyejua kumnyenyekea bwana, usiyojua mahaba, nakwambia utanitambua..."

Safari hii mpokeaji alibaki kimya akisikiliza maneno ya kejeli, dharau na vitisho vilivyokuwa vinatoka kwa mwanamke huyo ambaye alimpigia simu."

"Hivi wewe unanijua unanisikia, na siku nikikutana na wewe..." Ghafla akakata simu baada ya kuona dada aliyempigia simu akizidi kuporomosha mfululizo wa maneno ya karaha na vitisho.

Alibaki anahema kama mbwa aliyemkimbiza sungura kwa muda wa masaa matatu porini. Mchanganyiko wa mshangao na hasira vilimfanya aangue kilio. Kilikuwa ni kilio cha kwikwi. Akajiuliza ni nani aliyempigia simu? Ni mwanamke ambaye hajajitambulisha. Kwa maneno yake aliyokuwa anaongea anaonekana ni mwanamke ambaye huenda awali alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na mumewe, labda waliahidiana kuoana, lakini baadaye Dan akamuoa mwanamke mwingine ambaye ni yeye.

"Sasa kwa nini ananikasirikia? Ina maana bado anamtaka mume wangu?" Akajiuliza.

Anaitwa Husna, binti aliyezaliwa Manyoni mkoani Singida. Hakuwa mwenyeji wa mkoa huo ila alizaliwa kwa sababu baba yake mzazi ambaye alikuwa mwalimu wa shule ya msingi alihamishiwa huko kikazi. Baba yake alikuwa anatokea mkoani Iringa na mama yake Mwanza.

**Anaitwa Husna, binti aliyezaliwa Manyoni mkoani Singida. Hakuwa mwenyeji wa mkoa huo ila alizaliwa kwa sababu baba yake mzazi ambaye alikuwa mwalimu wa shule ya msingi alihamishiwa huko kikazi.**

Wakati yupo kidato cha kwanza, baba yake alifariki dunia, huku akiacha ugomvi mkubwa wa familia kugombea mirathi. Baada ya vitisho vya familia ya marehemu mumewe, mama Husna hakutaka tabu, aliamua kukusanya kilicho chake na mtoto wake mmoja Husna akarejea kwao Mwanza.

Hata hivyo hakuwa na uwezo wa kumsomesha tena. Mdogo wa mama yake, Tabia ambaye anafanya biashara ndogo ndogo za ujasiriamali jijini Dar es Salaam aliamua kumchukua.

Akawa anaishi naye maeneo ya Mburahati jijini Dar es Salaam. Akamaliza kidato cha nne, lakini hakuendelea tena baada ya hapo, hivyo alibaki akimsaidia mama yake mdogo kwenye biashara zake.

Husna alikuwa binti nzuri, aliyeumbwa na kuumbika. Ni mmoja wa wasichana ambao akipishana na mwanaume, hatokubali kumuangalia mara moja tu. Atataka amtazame tena na tena. Pia ni mmoja kati ya wasichana wachache waliojikubali walivyo bila kujikobeka madawa ya ngozi, au kujiremba kupita kiasi. Mama yake mdogo alikuwa mkali mno na kumpa semina kuhusu vijana wa mjini kuwa wangeweza kumharibia maisha. Akawa mtoto mtulivu mno. Kijana mmoja maeneo ya Mabibo alimuona Husna.

Akamhitaji. Hakutaka kumharibia maisha. Alikwenda kwao na kufuata taratibu zote, akafunga naye ndoa. Ndoa ilifungwa na kufana.

Hii ni miezi miwili tu, tayari siku zimeanza kupigwa simu za kumtisha. Wakati akitafakari na kufuta machozi, alisikia tena simu ikaita. Aliitazama kwa muda mrefu bila kupokea. Mawazo yakamjia ghafla kuwa huenda si yule dada, ni ya mtu mwingine. Alipotazama namba akaona ni ile ile. Haikuwa imeseviwa, lakini tayari alikuwa ameikariri. Mwisho ilikuwa na namba tano mbili.

Alitaka aikate. Lakini ghafla akaona bora aipokee, inawezekana huyo dada alikosea namba na sasa anataka kumuomba radhi. Akaichukua, akaiweza sikioni na kubonyeza kitufe, tayari kwa kusikiza kitakachoongeza.

"We bibie, mbona unakata wakati mwenzako sijamaliza? Yamekuingia ee, pole sana. Sasa nachokwambia ni hiki, hivi sasa huyo bwana unayeringia ninaye miye. Usishangae, ninaye hapa ndani hivi navyokueleza, najua anaoga nini, anakula nini, na anavaa vipi, ulidhani ukiolewa bwana atakuwa wa kwako peke yako ee, huyu hapa dada. Au nikupe simu uongee naye, hahahaha, utakufa kwa presha bure sikupi. Yaani umeolewa lakini bwana kaja kwangu, lo. Mwamke gani usiyojua kumlea mwanaume, mwanamke usiyejua kumnyeyekea bwana, mwanamke usiyojua mahaba, tena ninavyokwambia bwana ninaye miye, bwana yumo ndani anajilia vyake..." Husna akakata tena. mambo yalikuwa yamemzidi sasa. Akatamani aibamize simu ukutani, lakini nguvu hakuwa nazo mikononi. Akawa anatetemeka mwili mzima. Akalia zaidi ya mwanzo. Safari hii aliona huenda kinachoongewa hata kina asilimia kubwa ya ukweli.

Ni wiki mbili sasa tangu alipoagana na mumewe ambaye alimuaga kuwa anakwenda Zanzibar kikazi. Na amekuwa akiwasiliana naye kila siku, akiongea naye, akimpa moyo na matumaini kuwa baada ya wiki mbili tu atarejea nyumbani wafurahi pamoja.

"Kumbe yuko kwa hawara zake!" Akajikuta akiongea kwa sauti kubwa ya ukali. "Sasa kwanini ulinitoa kwetu, kwa mama yangu kuja kuniweka kwenye hatari hii Dan? Unawapa namba hawara zako wanitukane?" Akamuuliza mumewe ambaye hayupo. "Ngoja arudi, atanitambua!"

ITAENDELEA JUMAPILI





## Billnass akumbuka mengi machungu

MSANII wa Hip hop, William Lyimo, maarufu kama Billnass , amesema amejifunza mengi katika maisha ya rapa Golden Mbunda, aliyejulikana kwa jina la Godzilla.

Amesema katika maisha yake yote ya muziki kabla ya kufariki dunia, aligundua kazi ya muziki walioichagua wasanii ni ngumu sana.

"Mara zote ambacho najifunza kupitia marehemu Godzilla na baadhi ya vitu ambavyo nimeviona, nimebaini kazi ya sanaa ni ngumu, ina athari nyingi," alisema rapa huyo wakati akihojiwa na Salama Jabir kupitia YahStoneTown.

## VERA AJIFUNGUA MTOTO WA PILI

MREMBO anayepamba video za wanamuziki Afrika Mashariki, Vera Sidika, amewashangaza mashabiki wake baada ya kufichua jinsi ya mtoto wake wa pili.

Vera ni mahiri linapokuja suala la kiki na biashara ya sanaa, na hata katika suala la kujifungua watoto wake linampatia pesa nyingi.

Mlimbwende huyo alijifungua siku chache zilizopita, lakini alijizuia kumtambulisha mtoto wake huyo wa kiume kutokana na kutaka mauzo katika kipindi chake kinachozungumzia maisha yake.

Vera aliandaa sherehe ya aina yake katika kipindi chake cha Real Housewives Of Nairobi, msimu wa tatu na hapo ndipo mshiriki mwenzake Lisa Christoffersen, alipotoboa siri kuwa Vera ana mtoto.

"Vera angeweza kuwa hapa, lakini amejifungua mtoto tu. Sonal Merali yupo India kwa masuala ya familia," Lisa alijibu.

Baada ya muda, Vera alichapisha video na kufichua jinsi ya mtoto wake wa kiume, baada ya kurekodiwa awali kwa ajili ya shoo hiyo.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**MBAPPE ANUKIA MADRID**
REAL Madrid inamtaka Kylian Mbappe, lakini wanatumaini wanaweza kumsajili kwa uhamisho huru mara mkataba wake utakapomalizika kule PSG mwaka 2024. (***AS***)

**BENZEMA ATAFUTIWA MRITHI**
MSHAMBULIAJI wa Tottenham Hotspur na Brazil, Richarlison mwenye umri wa miaka 25, amejiunga na mshambuliaji wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe mwenye miaka 24 na Gonçalo Ramos wa Benfica mwenye umri wa miaka 21, kama mbadala wa mshambuliaji wa Ufaransa, Karim Benzema mwenye miaka 35 pale Real Madrid. (***Mundo Deportivo***)

**RICHARLISON KUMRITHI VLAHOVIC**
JUVENTUS inataka kumsajili Richarlison kama mbadala wa mshambuliaji wa Serbia, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 23, ambaye anatarajiwa kuondoka katika klabu hiyo ya Serie A msimu wa joto. (***Calciomercato***)

**PSG BAJETI EURO MIL 80**
KLABU ya PSG ina bajeti ya uhamisho ya euro milioni 80 pekee kwa msimu huu wa joto na wanatazamia kumuuza angalau mshambuliaji mmoja wa Brazil, Neymar mwenye umri wa miaka 31 na Lionel Messi mwenye miaka 35, katika jitihada za kupata fedha za kusajili wachezaji wapya. (***Goal***)

**MESSI KUTUA MAREKANI**
KLABU ya Inter Miami ya Ligi Kuu ya Marekani, MSL, inatumia "njia zote zinazowezekana" kumnasa Lionel Messi. (L'Equipe)

**RAYA HAUZWI**
KLABU ya Brentford haitamuuza mlinda mlango wa Hispania, David Raya mwenye umri wa miaka 27 msimu huu wa joto ikiwa hawatapokea ofa inayokubalika kwani wako tayari kumruhusu aondoke bila malipo mwaka wa 2024. (***90min***)

**FOREST KUSAJILI**
KLABU ya Nottingham Forest huenda ikafanya usajili mwingine mwishoni mwa msimu huu, huku kocha, Steve Cooper akitarajiwa kukabidhiwa bajeti ya zaidi ya pauni milioni 100 iwapo wataepuka kushushwa daraja kutoka Ligi Kuue. (***Football Insider***)

**BALEBA AGOMBEWA**
KLABU za Arsenal, Liverpool, Manchester United na Newcastle United ni miongoni mwa timu ambazo zimemtafuta kiungo wa kati wa Lille na Cameroon, Carlos Baleba mwenye umri wa miaka 19. (***90min***)

**MAN KUUZWA KABLA YA JUNI**
FAMILIA ya Glazer inalenga kuuzwa kwa Manchester United kabla ya dirisha la uhamisho kufunguliwa Juni. (Telegraph)

**KANE ALENGWA**
NAHODHA wa Tottenham Hotspur na England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 29, ndiye mshambuliaji mkuu anayelengwa na Manchester United msimu huu wa joto. (***Manchester Evening News***)

**TUCHEL HAITAKI SPURS**
KOCHA wa zamani wa Chelsea, Mjerumani Thomas Tuchel mwenye umri wa miaka 49 hatafikiria kuchukua nafasi ya Antonio Conte kama kocha wa Tottenham isipokuwa wakifuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya. (***Football Insider***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA




# GUARDIOLA: HAALAND ANAWEZA KUNG'ARA LIGI YOYOTE DUNIANI

## ●●● Asema kuanzia Ulaya, Amerika na hata Afrika atafunga mabao mengi na...

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola anaamini Erling Haaland anaweza kuzoea kucheza katika nchi yoyote baada ya msimu wa kwanza wa kuvutia kwenye Ligi Kuu ya England, EPL.

**City ilimsajili Haaland kutoka Borussia Dortmund ya Ujerumani, wakati hapo awali alicheza huko Austria katika timu ya Salzburg na Molde ya nyumbani kwao Norway.**

Ingawa uchezaji wake wa kiungo mara kwa mara umekosolewa, kipaji cha kufunga mabao cha Haaland kimemudu katika kila ligi.

Tayari ana mabao 27 kwenye Ligi Kuu msimu huu na ana rekodi ya kufunga mabao 34 kwa msimu mmoja, lakini Guardiola anatarajia itakuwa hadithi kama hiyo kama akienda kucheza kwenye Ligi nyingine.

Alipoulizwa kama alifaa zaidi kucheza England, Guardiola alijibu: "Naweza kusema anafaa popote kuanzia Ujerumani, Hispania, Italia, Norway, Congo na sehemu nyingine yoyote.

"Wachezaji wa aina hii hubadilika kila mahali; barani Afrika, Amerika Kusini, hakuna shida yoyote."

Idadi ya mabao ya Haaland inaweza kuwa ya kuvutia zaidi ikiwa Kevin De Bruyne atacheza kwa kiwango zaidi msimu huu.

Kauli ya Guardiola imekuja wakati Haaland akiendeleza kuhusishwa na kutakiwa na klabu kubwa barani Ulaya, huku Real Madrid ikiongoza kwenye mbio za kuwania saini yake.

Kwa mujibu wa ripoti ya Dail Mail, Madrid wanapanga kuwasilisha ofa ya kumsajili nyota huyo katika kipindi cha majira ya joto yajayo.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 508

MECHI KALI
MANCHESTER UTD
VERSUS
SOUTHAMPTON
1 | 1.37
X | 4.56
2 | 7.08

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# NEYMAR AFANYIWA UPASUAJI KWA MAFANIKIO

**PARIS,** Ufaransa

NEYMAR alifanyiwa upasuaji wa mafanikio kwenye jeraha lake la kifundo cha mguu Ijumaa, klabu yake ya Paris Saint-Germain imetangaza.

Mbrazil huyo amekuwa nje ya uwanja tangu alipotolewa katika ushindi wa 4-3 wa Ligue 1 dhidi ya Lille mwezi uliopita.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 amekuwa akifurahia msimu wake wenye tija zaidi kwa PSG tangu kampeni ya 2018-19, sawa na hesabu ya kuhusika na mabao 34 (mabao 18, asisti 16) katika mashindano yote - akiwa wa pili kwa juu zaidi katika maisha yake ya PSG, nyuma ya 44 katika msimu wake wa kwanza.

PSG wameshinda michezo yao yote miwili ya Ligue 1 bila Neymar na hivyo kusonga mbele kwa pointi nane kileleni mwa msimamo, ingawa waliondolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kichapo cha 2-0 kutoka kwa Bayern Munich, Jumatano.

Kocha mkuu Christophe Galtier alithibitisha mapema wiki hii kwamba Neymar atakosa kipindi chote cha msimu kilichobakia, huku fowadi huyo akitarajiwa kuwa nje kwa miezi mitatu hadi minne.

Taarifa ya klabu iliyotolewa Ijumaa ilisomeka: "Neymar alifanyiwa upasuaji Ijumaa alfajiri katika Hospitali ya ASPETAR huko Doha, na Maprofesa, Pieter D'Hooghe, James Calder na Rodrigo Lasmar.

# Potter ataka Mount apewe mkataba mpya



**LONDON,** England

GRAHAM Potter amekiri mkataba wowote mpya wa Chelsea kwa Mason Mount lazima uwe sahihi kwa mchezaji huyo, ambaye amekuwa akihusishwa na kutaka kuondoka hapo Stamford Bridge.

Mkataba wa sasa wa Mount hapo Blues unamalizika mwishoni mwa msimu ujao na bado hawajafikia makubaliano ya mkataba mpya, na klabu kama Liverpool, Manchester United na Newcastle United wametajwa kumtaka kiungo huyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 amekosa mechi mbili za mwisho za Chelsea - akishinda Leeds United na Borussia Dortmund - kutokana na jeraha, ingawa alianza mechi moja tu kati ya nne za awali katika mashindano yote.

Potter alielezea nia yake ya kupata azimio la haraka kwa mazungumzo ya Mount na klabu mwezi uliopita, lakini bila maendeleo yoyote yanayoonekana, anakubali kwamba mchezaji huyo wa kimataifa wa England anaweza kuhitaji kuchukua muda wake.

"Mwishowe ni kati ya klabu na Mason," alisema Potter Ijumaa. "Nimezungumza naye mara nyingi kuhusu hali yake, soka na maisha kwa ujumla.

"Hisia zangu kwa Mason ziko wazi. Yeye ni mtu wa ajabu kwanza, lakini wakati mwingine mambo haya hutokea.

"Ni ngumu tu na ni bora nizungumze kidogo juu yake, wacha waendelee nayo katika kuamua ni nini kinafaa kwa pande zote mbili.

" Najua ni wakati muhimu kwake na mkataba muhimu. Mambo haya yanapaswa kuwa sawa kwake na familia yake. Ni muhimu kufanya uamuzi kwa msingi huo."

Mount ameichezea Chelsea mechi 32 msimu huu, 26 kati ya hizo alianza, huku akichangia mabao sita, akipitwa na Raheem Sterling (10) na Kai Havertz (nane) katika msimu huu unaonekana kuwa mbaya kwa The Blues hao.

,027,160

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 14/03/23 | 23:00 | Porto vs Inter | 2.60 | 3.30 | 2.49 |
| 02. 15/03/23 | 02:05 | Tlaxcala FC vs Venados FC | 2.58 | 3.15 | 2.53 |
| 03. 15/03/23 | 04:10 | Independiente Santa Fe vs America De Cali | 2.27 | 3.06 | 3.01 |
| 04. 15/03/23 | 06:05 | Correcaminos Uat vs Tepatitlan FC | 2.24 | 3.11 | 3.01 |
| 05. 15/03/23 | 19:30 | NK Celje vs Olimpija Ljubljana | 2.62 | 3.23 | 2.39 |
| 06. 15/03/23 | 22:30 | Southampton vs Brentford | 2.85 | 3.15 | 2.38 |
| 07. 15/03/23 | 23:00 | Real Madrid vs Liverpool | 2.33 | 3.46 | 2.68 |
| 08. 16/03/23 | 20:45 | Fenerbahce vs Sevilla FC | 2.23 | 3.37 | 3.16 |
| 09. 16/03/23 | 20:45 | Djurgardens IF vs Lech Poznan | 2.46 | 3.27 | 2.72 |
| 10. 16/03/23 | 20:45 | Slovan Bratislava vs FC Basel | 2.47 | 3.23 | 2.73 |
| 11. 16/03/23 | 23:00 | AZ Alkmaar vs Lazio | 2.83 | 3.28 | 2.37 |
| 12. 16/03/23 | 23:00 | Union Saint Gilloise vs Union Berlin | 2.77 | 3.32 | 2.39 |
| 13. 16/03/23 | 23:00 | Real Sociedad vs Roma | 2.19 | 3.27 | 3.32 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 12/03/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 4165 | Ankaragucu vs Alanyaspor | 2.33 | 3.36 | 2.79 |
| 14:00 | 5816 | Zenit St Petersburg vs FK Khimki | 1.10 | 7.74 | 19.87 |
| 14:15 | 3433 | NEC Nijmegen vs Utrecht | 2.37 | 3.20 | 2.80 |
| 14:30 | 4159 | Lecce vs Torino | 2.84 | 2.89 | 2.55 |
| 15:00 | 2953 | Clermont Foot vs Lens | 4.20 | 3.35 | 1.81 |
| 16:00 | 3133 | Aswan vs Coca Cola | 3.48 | 3.08 | 2.12 |
| 16:00 | 3994 | Mallorca vs Real Sociedad | 3.26 | 2.81 | 2.34 |
| 16:00 | 4024 | Trabzonspor vs Adana Demirspor | 1.69 | 3.73 | 4.42 |
| 16:30 | 3742 | Heerenveen vs Ajax | 5.99 | 4.59 | 1.42 |
| 17:00 | 1681 | West Ham vs Aston Villa | 2.16 | 3.19 | 3.19 |
| 17:00 | 2036 | Fulham vs Arsenal | 4.93 | 3.74 | 1.61 |
| 17:00 | 2641 | Manchester Utd vs Southampton | 1.37 | 4.56 | 7.08 |
| 17:00 | 4535 | AC Ajaccio vs Montpellier | 2.86 | 3.06 | 2.42 |
| 17:00 | 4699 | Verona vs Monza | 2.44 | 3.10 | 2.80 |
| 17:00 | 4971 | Angers vs Toulouse | 3.40 | 3.55 | 1.95 |
| 17:00 | 4990 | Cremonese vs Fiorentina | 4.00 | 3.50 | 1.80 |
| 17:00 | 5153 | Nantes vs Nice | 2.85 | 3.05 | 2.43 |
| 17:00 | 5811 | Lorient vs Troyes | 1.72 | 3.69 | 4.19 |
| 17:30 | 5548 | SC Freiburg vs Hoffenheim | 1.88 | 3.46 | 3.71 |
| 18:00 | 3666 | Horsens vs Copenhagen | 6.50 | 4.06 | 1.48 |
| 18:15 | 2266 | Young Africans vs Geita Gold FC | 1.12 | 4.50 | 7.50 |
| 18:15 | 5084 | Sevilla FC vs Almeria | 1.62 | 3.74 | 4.89 |
| 18:30 | 1036 | Grasshoppers vs FC Winterthur | 2.13 | 3.36 | 3.15 |
| 18:30 | 1037 | Rio Ave vs Gil Vicente | 2.36 | 3.16 | 2.91 |
| 18:45 | 5116 | PSV Eindhoven vs Cambuur | 1.13 | 7.20 | 15.01 |
| 19:00 | 1874 | Sturm Graz vs Austria Vienna | 1.69 | 3.65 | 4.11 |
| 19:00 | 2274 | Basaksehir vs Besiktas | 2.68 | 3.21 | 2.49 |
| 19:00 | 2937 | LASK Linz vs RB Salzburg | 3.17 | 3.43 | 1.99 |
| 19:00 | 3263 | Wolfsberger AC vs Austria Lustenau | 1.75 | 3.60 | 3.85 |
| 19:00 | 4944 | Rapid Vienna vs WSG Wattens | 1.60 | 3.80 | 4.51 |
| 19:05 | 3485 | Monaco vs Reims | 1.79 | 3.65 | 3.90 |
| 19:30 | 1045 | Werder Bremen vs Bayer Leverkusen | 3.09 | 3.59 | 2.05 |
| 19:30 | 2642 | Newcastle vs Wolverhampton | 1.63 | 3.64 | 4.99 |
| 20:00 | 1559 | Panetolikos vs Lamia | 2.23 | 3.02 | 3.39 |
| 20:00 | 2804 | Volos vs PAOK | 8.28 | 4.35 | 1.38 |
| 20:00 | 4275 | Roma vs Sassuolo | 1.65 | 3.56 | 4.91 |
| 20:00 | 4550 | AEK Athens vs Olympiakos | 2.05 | 3.23 | 3.61 |
| 20:00 | 4903 | Aris Salonica vs PAS Giannina | 1.48 | 3.98 | 6.80 |
| 20:00 | 5625 | Atromitos vs Panathinaikos | 7.03 | 3.68 | 1.51 |
| 20:30 | 3180 | Villarreal vs Betis | 1.85 | 3.51 | 3.76 |
| 20:30 | 5995 | Racing Genk vs Union Saint Gilloise | 2.24 | 3.32 | 2.96 |
| 21:00 | 4445 | Maritimo vs Benfica | 10.06 | 5.43 | 1.25 |
| 21:15 | 1609 | Hapoel Beer Sheva vs Ironi Kiryat Shmona | 1.32 | 4.30 | 6.60 |
| 21:30 | 1563 | VfL Wolfsburg vs Union Berlin | 2.20 | 3.14 | 3.14 |
| 22:00 | 2043 | Steaua Bucuresti vs Sepsi Osk | 2.01 | 3.35 | 3.40 |
| 22:00 | 4254 | Feyenoord vs FC Volendam | 1.12 | 7.78 | 14.97 |
| 22:45 | 2914 | Marseille vs Strasbourg | 1.38 | 4.52 | 6.82 |
| 22:45 | 4997 | Juventus vs Sampdoria | 1.38 | 4.18 | 7.98 |
| 23:00 | 1949 | Athletic Bilbao vs Barcelona | 3.15 | 3.10 | 2.22 |
| 23:30 | 1390 | Sporting Lisbon vs Boavista | 1.23 | 5.59 | 10.97 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# BMT YATOA SOMO KWA WANARIADHA TANZANIA

**Na Saada Akida**

KATIBU Mtendaji wa Baraza la Michezo la Tanzania (BMT), Neema Msitha amewataka wanariadha wa Afrika Mashariki (EEAR) kuendelea kufanya mazoezi kwa bidii na kutambua ni jukumu lao la msingi. Neema alizungumza hayo juzi katika Mashindano ya Riadha ya Vijana chini ya umri wa miaka 18 na 20 kutoka mataifa mbalimbali huku Tanzania wakiwa wenyeji wa mashindano hayo.

Alisema mashindano hayo yanasaidia kutengeneza vipaji ambavyo vitaandaliwa kwa ajili ya kuleta medali kimataifa kwa miaka ijayo kwenye mashindano ya Afrika na dunia.

"Mashindano haya ya vijana ni ya msingi kuliko ya wakubwa kwa sababu tunayapa kipaumbele kutokana na wakubwa wanastaafu hivi karibuni, huu ni muda muafaka wa kuwaandaa vijana hawa," alisema Neema.

Aliongeza; "Vijana msijute hapo mlipo, kuna manufaa makubwa watu wanaishi Ulaya na maeneo mbalimbali kupitia michezo, mtumie ujana wenu wa kati kwa sasa kujitengenezea maisha ya baadae."

Aliwashukuru wadau kutoka nchini Kenya ambao wametoa kifaa kinachoshughulikia hali ya hewa kwa wachezaji na wananchi wa Wilaya ya Temeke.

"Hiki kifaa ni muhimu kuwepo katika mashindano makubwa kama haya yanayoendelea sasa, lazima kifaa hicho kiwepo upate fursa ya kuandaa mashindano ya Kimataifa," alisema.

Alisema kwa sasa Serikali ipo kwenye mchakato wa kuboresha miundombinu ya uwanja wa Benjamini Mkapa kwa kuhakikisha unakuwepo kwa vifaa muhimu ikiwemo hicho cha kujua hali ya hewa ya wanamichezo wanaoshiriki.

Wakati huo huo, Makamu wa Rais wa Shirikisho la Riadha Tanzania (RT), William Kallaghe amepokea hundi ya Sh. milioni tatu kutoka kwa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) ambayo itatumika kwa ajili ya kuwandaa kushiriki mashindano ya vijana chini ya umri wa miaka 18 na 20 ya Afrika mwaka huu.

"Benki ya NBC ndio mdhamini pekee wa kimkakati aliyejitokeza kuunga mkono na itakuwa kivutio kwa wadau wengine kuja kwa wingi kutusaidia kwa kutupa mchango wao," alisema Kallaghe.



Mchezaji wa timu ya Iman Veteran, Hashim Abdallah, akiokoa mpira wa juu uliokuwa umeelekezwa golini kwao huku akizongwa na wachezaji wa Stakshari Veteran katika mchezo wa Bonanza lililofanyika Kitunda Kivule jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Yanga kazi moja tu kwa Geita leo

INATOKA UK 24

ugumu wa Geita Gold ambao tulikutana nao mechi ya kwanza na ilikuwa ngumu na tunahitaji kupata matokeo ya kupata pointi tatu, tumewaandaa vizuri wachezaji wetu kiufundi na kiakili," alisema.

"Tunaelekea ukingoni mwa ligi na lazima kesho (leo) tupate pointi tatu muhimu ili hapo baadae tusicheze kwa presha kubwa."

Kaze alisema Tuisila Kisinda hataweza kucheza kwani amepata maumivu na anaendelea kufanyiwa vipimo kuona kama ameumia kwa kiasi kikubwa, huku Jesus Moloko pia hayuko fiti na bado wanamuangalia, na Salum Abubakari amerejea katika kikosi baada ya kupata matatizo ya kifamilia.

Mwakilishi wa wachezaji wa Yanga, Fiston Mayele alisema wamejiandaa vizuri katika mechi ya leo na wachezaji wanahitaji kupata matokeo mazuri licha ya mechi hiyo kuwa ya ushindani mkubwa.

"Benchi la ufundi limefanya kazi kubwa kufanya maandalizi, majukumu makubwa yako kwetu kupambana tunashinda mechi ya kesho (leo) kupata pointi tatu za Geita Gold FC na zilizopo mbele yetu.

Ufungaji bora kwa sasa ni mapema kwanza Yanga halafu mimi baadae, nahitaji kusaidia timu kutwaa taji hili kwa kuendelea kufunga pale ninapopata nafasi ya kufunga na mwisho wa siku nitimize malengo ya kuibuka mfungaji bora," alisema Mayele.

Kuelekea mchezo huo Kocha Msaidizi wa Geita Gold, Mathias Wandiba alisema maandalizi yako vizuri kwa kuandaa wachezaji kisaikolojia kiufundi na kimbinu.

Alisema kikosi kimeimarika kwa ajili ya kwenda kupambana kutafuta matokeo mazuri katika mchezo huo wa leo ili kuendelea kujiweka kwenye nafasi nzuri katika msimamo wa ligi kuu.

"Tunatambua itakuwa mechi ya ushindani mkubwa kwa sababu Yanga ni timu kubwa na imetoka kushinda katika michuano ya kimataifa, kimbinu na ufundi tuko vizuri na ninaimani tunaenda kuonyesha mpira mzuri," alisema Wandiba.

Alisema wachezaji waliosafiri kuja nao Dar es Salaam wote wako fiti na wanashuka dimbani kivingine kusaka alama tatu katika mchezo huo ambao watacheza kwa tahadhari kubwa.

Nahodha wa Geita Gol FC, Geoffrey Manyac alisema wamejiandaa vizuri na kila mmoja wao yuko tayari kwenda kupambana kutafuta matokeo chanya.

"Tunatambua utakuwa mchezo mgumu na ushindani kikubwa tumejiandaa vizuri na tayari kwenda kusaka pointi tatu, tumeandaliwa vizuri kuwakabili Yanga," alisema Manyasi.

# Michezo

Nipashe

Jumapili Machi 12, 2023






Neymar afanyiwa upasuaji kwa mafanikio




Jean Baleke akifunga bao la pili la Simba wakati wa mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Mtibwa Sugar jana kwenye Uwanja wa Manungu, Turiani Morogoro. **PICHA: SIMBA**

## Yanga kazi moja tu kwa Geita leo

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Yanga kinashuka dimbani leo kusaka pointi tatu dhidi ya Geita Gold FC kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, utakaopigwa katika uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam.

Yanga wanahitaji kupata matokeo mazuri ili kuendelea kujiimarisha kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo huku wakiivaa Geita Gold iliyopo nafasi ya tano wakiwa na alama 34.

Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze alisema wanajua umuhimu wa mechi kwa sababu wanaelekea ukingoni mwa ligi na hivyo watacheza kwa tahadhari kubwa.

Alisema watacheza kwa malengo ya kusaka pointi tatu, na wanatambua haitakuwa rahisi licha ya wachezaji wao kuwa fiti baada ya kucheza michezo mfululizo hivi karibuni.

"Tumejipanga vizuri na tunatambua

INAENDELEA UK 23

# Simba yairarua Mtibwa

## Baleke atupia 'hat-trick' ya mapema zaidi Ligi Kuu, yafikisha pointi 57 yawasogelea...

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Simba, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Jean Baleke aliyesajiliwa kipindi cha dirisha dogo aliyekuwa akicheza kwa mkopo kwenye klabu ya Nejmeh SC ya Lebanon kutoka TP Mazembe, jana alifunga 'hat-trick' yake ya kwanza kwenye Ligi Kuu ya Tanzania, akiiwezesha timu yake kushinda bao 3-0 dhidi ya Mtibwa Sugar.

Ameweka rekodi ya kufunga 'hat-trick' ya mapema zaidi kwenye Ligi Kuu, kwani mabao yote amefunga kipindi cha kwanza, dakika ya tatu, saba na 31.

Hiyo ni 'hat-trick' ya tano kwenye Ligi Kuu ya Tanzania Bara mpaka sasa, huku Simba ikiwa na 'hat-trick' nne, na Yanga moja, lakini zote hizo mabao mengine yalifungwa kipindi cha pili.

**Baleke anakuwa ni mchezaji wa tatu wa Simba kufunga 'hat-trick', wengine wakiwa ni nahodha John Bocco aliyefunga mbili dhidi ya Ruvu Shooting na Prisons, na Saido Ntibazonkiza aliyefunga dhidi ya Prisons.**

Kwenye pambano hilo lililochezwa Uwanja wa Manungu Complex, Turiani, mkoani Morogoro, alifunga bao la kwanza baada ya mpira wa kichwa uliopigwa na Moses Phiri, ambao ulianguka nyuma ya mabeki wa Mtibwa Sugar, akauwahi na kuukwamisha wavuni kwa mguu wa kulia, dakika ya tatu ya mchezo.

Dakika nne baadaye alifunga bao la pili lililotokana na mpira wa kona fupi iliyopigwa na Clatous Chama, kwake Ntibazonkiza, ambaye aliumimina langoni, Baleke akauchupia na kuupiga kichwa cha mbizi, mpira ukatuama wavuni.

Inakuwa na 'assist' ya tisa kwa Ntibazonkiza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Baleke alikamilisha 'hat-trick' yake dakika ya 33, baada ya faulo ndefu iliyopigwa na Sadio Kanoute ikamkuta Shomari Kapombe.

Kipa wa Mtibwa, Sugar Razack Shekimweri alimkimbia Kapombe kutaka kuuwahi mpira adake kabla hajapigwa kichwa, lakini alichelewa, kwani beki huyo wa kulia aliuwahi akaupiga mithili ya krosi kwenye lango lililokuwa limejaa mabeki bila kipa, mfungaji akafunga kwa staili ile ile ya bao la pili, kichwa cha mbizi.

Baada ya mabao hayo Simba ilionekana kuridhika na mabao na kupunguza kasi yake ya awali, huku ikirejea kucheza soka lake la pasi fupi fupi na taratibu, badala ya lile la mwanzo la kasi na pasi ndefu kwenda kwenye wingi zote mbili.

Kipindi cha pili Mtibwa Sugar ilifanya mabadiliko kadhaa, ikiwatoa kiungo aliyewahi kuichezea Simba zamani, Mghana, James Kotei na Vitalis Mayanga, wakiwaingiza Eliuter Mpepo, Onesmo Mayaya na George Chota mabao kwa kiasi kikubwa waliibadilisha timu hiyo hasa kwenye kiungo na kuanza kuwadhibiti viungo wa Simba.

Ni muda huo huo tu baada ya kuingia, dakika ya 54, Chota aliupata mpira akiwa kwenye eneo la hatari, akaachia shuti kali lililotoka nje kidogo ya lango.

Mpepo, ilikuwa karibu aiandikie Mtibwa walau bao la kufutia machozi, aliunganisha krosi ya Mayaya, kipa Aishi Manula aliudaka, lakini mpira ukamponyoka, lakini aliinuka na kuuwahi tena kuukamata kabla haujavuka mstari wa goli.

Simba ingeweza kuondoka na mabao zaidi ya matano, kama Saido angekuwa makini, kwani alipoteza nafasi nne za ambazo zingeweza kuwa mabao.

Straika chipukizi wa Simba, Mohamed Mussa, ambaye alifunga bao kwenye mechi ya Kombe la FA dhidi ya African Sports, nusura apachike bao kwenye mechi ya jana dakika za mwisho za mchezo, baada ya kuwahadaa mabeki wa Mtibwa Sugar na kuachia shuti ambalo lilimpita kipa Kimweri, lakini mpira ukapaa kidogo juu la lango.

Mchezaji huyo aliingia dakika 10 za mchezo kabla ya kumalizika pamoja na kina Peter Banda, Erasto Nyoni, na Habib Kyombo.

Matokeo hayo yanaifanya Simba kufikisha pointi 57, ikiendelea kuwa kwenye nafasi ya pili, Mtibwa ibaki kwenye nafasi ya tisa na pointi zake 29.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >